# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

## RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA USTAWI WA JAMII YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

**FEBRUARI, 2022**

# YALIOMO

YALIOMO .... 2
SEHEMU YA KWANZA .... 6
1. UTANGULIZI .... 6
1.1 MUUNDO WA KAMATI .... 7
1.2 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI .... 8
1.3 HADIDU REJEA .... 9
**SEHEMU YA PILI** .... 9
**2. WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO** .... 10
**A. UTANGULIZI** .... 10
**IDARA:** .... 10
**TAASISI** .... 11
**MABARAZA YA KITAALUMA/BODI** .... 11
**B. PROGRAMU YA HOSPITAL YA MNAZI MMOJA** .... 11
HOSPITALI YA MNAZI MMOJA .... 12
**CHANGAMOTO ZA HOSPITALI YA MNAZIMMOJA** .... 12
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZOYA KAMATI .... 13
**C. PROGRAMU YA TIBA** .... 14
I. PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU .... 14
**TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)** .... 14
**CHANGAMOTO ZA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)** .... 15
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .... 15
**BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA** .... 17
**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA** .... 17
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .... 18
**BARAZA LA MADAKTARI ZANZIBAR** .... 18
**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MADAKTARI ZANZIBAR** .... 19
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .... 19
HOSPITALI ZA WILAYA MICHEWENI, WETE, KIVUNGE NA MAKUNDUCHI .... 20
CHANGAMOTO ZA HOSPITALI ZA WILAYA MICHEWENI, WETE, KIVUNGE NA MAKUNDUCHI .... 21
**KITUO VYA MKONO KWA MKONO HOSPITAL YA MICHEWENI, MAKUNDUCHI PAMOJA NA WETE** .... 23
**CHANGAMOTO ZA VITUO VYA MKONO KWA MKONO** .... 24
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .... 25
WARATIBU WA SHEHIA WANAOSHUGHULIKIA MASUALA YA VITENDO VYA UKATILI NA UDHALILISHAJI WA WANAWAKE NA WATOTO .... 27
CHANGAMOTO ZA WARATIBU WA SHEHIA .... 28
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI .... 29
**BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR** .... 30
**CHANGAMOTO ZA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR** .... 30
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .... 31
**II. PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA NA UCHUNGUZI** .... 34
**WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR** .... 34
**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI** .... 34
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .... 35

**WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI** ... 36
**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI** ... 36
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ... 38
KITENGO CHA KUPAMBANA NA UDHIBITI WA MAJANGA YA DHARURA YA KIAFYA ZANZIBAR ... 39
MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA KUANZISHWA KITUO CHA KUPAMBANA NA UDHIBITI WA MAJANGA YA DHARURA YA KIAFYA ZANZIBAR ... 40
CHANGAMOTO ZA KITENGO CHA KUPAMBANA NA UDHIBITI WA MAJANGA YA DHARURA YA KIAFYA ZANZIBAR ... 41
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ... 41
**D. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** ... 42
**MAFANIKIO YA PROGRAMU** ... 42
**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA** ... 43
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ... 44
**3. WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI** ... 48
IDARA ... 48
MABARAZA NA BODI ... 48
A. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU ... 49
**CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)** ... 50
**CHANGAMOTO ZA CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)** ... 51
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ... 53
**TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA** ... 54
**LENGO KUU LA KUANZISHWA KWA TAASISI** ... 55
**CHANGAMOTO ZA TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA** ... 56
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ... 57
**B. PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU** ... 58
AFISI YA MRAJIS WA ELIMU ... 59
CHANGAMOTO ZA AFISI YA MRAJIS WA ELIMU ... 59
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ... 60
BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR ... 60
CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR ... 61
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ... 61
**OFISI YA MKAGUZI WA ELIMU ZANZIBAR** ... 62
**CHANGAMOTO ZA OFISI YA MKAGUZI WA ELIMU ZANZIBAR** ... 62
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ... 64
**KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA** ... 65
**CHANGAMOTO ZA KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA** ... 65
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** ... 66
**C. PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA** ... 67
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI ... 68
4. WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO ... 73
SEKTA YA HABARI ... 74
SEKTA YA VIJANA ... 74

SEKTA YA UTAMADUNI .......... 74
SEKTA YA MICHEZO .......... 74
IDARA YA MIPANGO, SERA NA UTAFITI .......... 74
IDARA YA UTUMISHI NA UENDESHAJI .......... 74
AFISI KUU PEMBA .......... 74
A. PROGRAMU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI ... 75
I. PROGRAMU NDOGO YA UPATIKANAJI NA USAMBAZAJI WA HABARI ....... 75
SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (*ZBC*) .......... 75
MAJUKUMU YA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC) .......... 75
CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (*ZBC*) .......... 76
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... 77
SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR .......... 78
CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR .......... 78
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI .......... 80
**KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX)** .......... 81
**CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX)** .......... 82
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... 82
**II. PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA VYOMBO VYA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI** .......... 83
**WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR** .......... 83
**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA UCHAPAJI ZANZIBAR** .......... 84
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... 85
**B. PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIJANA** .......... 86
BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR .......... 87
MAJUKUMU YA BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR .......... 87
CHANGAMOTO ZA BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR .......... 88
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI** .......... 88
MRADI WA "GREEN HOUSE" .......... 89
CHANGAMOTO ZA MRADI WA "GREEN HOUSE" .......... 90
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI .......... 90
**D. PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO** . 91
**I. PROGRAMU NDOGO YA UIMARISHAJI, UHIFADHI, UBUNIFU NA UENDELEZAJI WA UTAMADUNI NA SANAA** .......... 91
AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI .......... 92
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI .......... 93
BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR (BAKIZA) .......... 94
CHANGAMOTO ZA BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR (BAKIZA) .......... 96
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI .......... 96
BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI (BASSFU) .......... 97
CHANGAMOTO ZA BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI (BASSFU) .......... 98
MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI .......... 99
**C. PROGRAMU KUU YA UTAWALA, UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** .......... 100

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**................................ 100
**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**........................................... 101
SEHEMU YA TATU........................................................................................................ 103
HITIMISHO................................................................................................................... 103

# SEHEMU YA KWANZA

## 1. UTANGULIZI

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi ni moja wapo ya Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya kifungu cha 85 cha Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 na Kanuni ya 107(1) ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, (Toleo la 2020).

Kazi na majukumu ya Kamati hii yamebainishwa na kufafanuliwa kwenye Jadweli la Kwanza la Kanuni za Baraza la Wawakilishi kama ifuatavyo:-

*(a)* Kufuatilia utekelezaji wa Maagizo ya Kamati yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka uliotangulia;

*(b)* Kufuatilia utekelezaji wa Sera na Mipango ya Wizara husika kwa kadri Spika atavyoelekeza kwa mujibu wa malengo yaliyowasilishwa Barazani wakati wa usomaji wa Bajeti na hotuba nyengine za Waziri alizotoa katika Baraza;

*(c)* Kufuatilia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitaifa na Miradi ya Wananchi katika Wizara husika;

*(d)* Kuchunguza na kufuatilia Mapato na Matumizi ya kila mwaka ya Serikali na kama matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha;

*(e)* Kuchambua Mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka;

*(f)* Kushughulikia Miswada ya Sheria inayokabidhiwa kwake na Spika;

*(g)* Kuchambua ahadi zote za Wizara zilizo chini ya Kamati kama zitakavyokuwa zikitolewa katika Baraza na kufuatilia utekeleaji wa ahadi hizo; na

*(h)* Kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kamati ya Kudumu ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar, katika Ripoti hii inajulikana kama "Kamati" ambapo ina jukumu la kufuatilia utekelezaji wa Wizara tatu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, ikiwa ni pamoja na Idara, Mashirika, Wakala, Mabaraza na Vitengo vilivyo chini ya Wizara hizo. Wizara hizo ni hizi zifuatazo:-

*(a)* Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto;

*(b)* Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali; na

*(c)* Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo.

## 1.1 MUUNDO WA KAMATI

Kamati hii inaundwa na Wajumbe wafuatao:-

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| **1.** | Mhe. Mohamed Ahmada Salum | Mwenyekiti |
| **2.** | Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | Makamu Mwenyekiti |
| **3.** | Mhe. Abdalla Abass Wadi | Mjumbe |
| **4.** | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| **5.** | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| **6.** | Mhe. Shaaban Ali Othman | Mjumbe |
| **7.** | Mhe.  Zawadi Amur Nassor | Mjumbe |

Aidha, Kamati hii inafanya kazi zake kwa kushirikiana na Makatibu na Msaidizi wa Mjumbe wafuatao:-

| Nam. | Jina | Wadhifa |
|---|---|---|
| **1.** | Ndg. Fatma Omar Ali | Katibu |
| **2.** | Ndg. Mussa Issa Mussa | Katibu |
| **3.** | Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi |

## 1.2 MALENGO YA KAZI NA MUDA WA KAZI ZA KAMATI

Kwa mwaka wa fedha 2020/2021, Kamati ilitekeleza kazi zake kwa malengo yafuatayo:-

*(a)* Kufuatilia Maagizo yaliyotolewa katika Ripoti ya Kamati ya mwaka 2019/2020.

*(b)* Kufuatilia ahadi za Serikali zilizotolewa katika Mkutano wa Bajeti wa mwaka 2019/2020.

*(c)* Kufuatilia utekelezaji wa Bajeti (kazi za kawaida na kazi za maendeleo) ya mwaka 2021/2022.

*(d)* Kufuatilia ukusanyaji wa mapato katika vitengo vya Serikali pamoja na kufanya ziara katika taasisi husika.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Kamati ilifanya kazi zake kwa muda wa wiki tano kama ifuatavyo:-

*(i)* Unguja, kuanzia tarehe 18/01/2021 hadi tarehe 29/01/2021.

*(ii)* Unguja na Pemba kuanzia tarehe 29/03/2021 hadi tarehe 10/04/2021.

*(iii)* Pemba na Unguja kuanzia tarehe 09/08/2021 hadi tarehe 20/08/2021.

*(iv)* Unguja na Dar-es-Salaam, kuanzia tarehe 08/11/2021 hadi tarehe 19/11/2021.

*(v)* Unguja na Pemba, kuanzia tarehe 17/01/2022 hadi tarehe 28/01/2022.

## 1.3 HADIDU REJEA

Katika Utekelezaji wa kazi kwa mwaka 2021/2022, Kamati ilitumia hadidu rejea zifuatazo:-

*(a)* Kanuni za Baraza la Wawakilishi Zanzibar, Toleo la Mwaka 2020.

*(b)* Taarifa Rasmi za Baraza 'Hansard' za Baraza za Mwaka 2019/2020.

*(c)* Ripoti za Kamati kwa Mwaka 2019/2020.

*(d)* Hotuba za Bajeti za Taasisi za Serikali zinazosimamiwa na Kamati hii.

# SEHEMU YA PILI

## 2. WIZARA YA AFYA, USTAWI WA JAMII, WAZEE, JINSIA NA WATOTO

### A. UTANGULIZI

Kamati katika kipindi chote cha kazi zake imefanyakazi ya kusimamia utekelezaji wa bajeti inayotumia muundo wa programu katika utekelezaji wake, ambapo kwa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa mwaka wa fedha 2021/2022, Wizara hii ilitekeleza na programu zifuatazo:-

*(i)* Programu ya Kinga na Elimu ya Afya;
*(ii)* Programu ya Tiba;
*(iii)* Programu ya Hifadhi ya Jamii, Maendeleo ya Jinsia na Watoto;
*(iv)* Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara; na
*(v)* Programu ya Hospitali ya Mnazi mmoja.

Programu hizo zinatekelezwa kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto, ambapo jumla ya Idara Saba (7), Taasisi sita (6) na Mabaraza saba (7) ya Taaluma mbali mbali za Kiafya kama ifuatavyo:-

**IDARA:**

*(i)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
*(iii)* Idara ya Kinga na Elimu ya Afya;
*(iv)* Idara ya Mfamasia Mkuu wa Serikali;
*(v)* Idara ya Bohari Kuu ya Dawa;
*(vi)* Idara ya Ustawi wa Jamii na Wazee; na

*(vii)* Idara ya Jinsia na Watoto.

**TAASISI**

*(i)* Hospitali ya Mnazi Mmoja;

*(ii)* Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi;

*(iii)* Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;

*(iv)* Maabara ya Afya ya Jamii - Pemba; na

*(v)* Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar.

**MABARAZA YA KITAALUMA/BODI**

*(i)* Baraza la Wauguzi na Wakunga;

*(ii)* Baraza la Madaktari;

*(iii)* Baraza la Tiba Asili na Tiba Mbadala;

*(iv)* Baraza la Afya ya Jamii;

*(v)* Baraza la Wataalamu wa Afya ya Mazingira;

*(vi)* Baraza la Wataalamu wa Maabara za Afya; na

*(vii)* Bodi ya Ushauri wa Huduma za Hospitali Binafsi.

Katika kufuatilia utekelezaji wa Programu hizo, Kamati ilifanya ziara katika Hospitali na Taasisi mbali mbali kwa lengo la kuona mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa Programu zilizopangwa pamoja na kubaini changamoto mbali mbali zinazokwamisha utekelezaji wa shughuli katika sehemu hizo na kuziwasilisha Serikalini kwa kuishauri Serikali namna bora itakayoweza kutumika katika kuzipatia ufumbuzi wa kudumu.

**B. PROGRAMU YA HOSPITAL YA MNAZI MMOJA**

## HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Hospitali ya Mnazi Mmoja ni Hospitali inajulikana kama Wakala wa Serikali kufuatia kupitishwa kwa Sheria Nam. 3 ya mwaka 2016. Hospitali hii ndio pekee hapa Zanzibar inayotoa Huduma za Rufaa kupitia Bodi ya Ushauri ya Hospitali ikiwa na lengo la kuimarisha huduma za uchunguzi, matibabu, tafiti na kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wa kada za afya.

## CHANGAMOTO ZINAZOIKABILI HOSPITALI YA MNAZI MMOJA

Hospitali hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Uhaba wa rasilimali watu hasa kwenye Idara ya Radioloji, fundi majengo, na fundi sanifu dawa wenye ujuzi;

*(b)* Upungufu wa vifaa vya utabibu wa mifupa na upungufu wa baadhi ya dawa na vifaa tiba;

*(c)* Kuharibika mara kwa mara kwa mashine ya “Haematology”;

*(d)* Kukosekana kwa dawa kutoka MSD ambaye ndiye msambazaji mkuu;

*(e)* Uhaba wa Madaktari Bingwa wa Kada tofauti za Afya katika Hospitali ya Rufaa, wakiwemo “Radiographer”; hakuna Daktari mwenye taaluma ya masuala ya Akili;

*(f)* Ufinyu wa bajeti wanayoingiziwa kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango nje ya makadirio waliyopangiwa, ambapo kwa robo ya mwaka Hospitali ya Mnazimmoja inatakiwa kutumia shilingi milioni 400 kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli za Hospitali ya Mnazi Mmoja, lakini kwa sasa kwa kila robo ya mwaka wanaingiziwa shilingi milioni 100 tu, hali

inayoipelekea kufanya kazi katika mazingira magumu na kukosekana kwa huduma muhimu zinazohitajika kutolewa katika hospitali hiyo.

*(g)* Maslahi madogo kwa madaktari pamoja na watendaji wa afya, hali inayowasababisha kuhama katika Hospitali ya Mnazi Mmoja na kukimbilia Hospitali Binafsi;

*(h)* Uwepo wa madeni makubwa kwa makampuni tofauti yanayotoa huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja. Kamati imepata taarifa kuwa hadi kufikia Disemba, 2021 Hospitali ya Mnazi Mmoja inadaiwa shilingi milioni 270;

*(i)* Uhaba wa mitungi ya "Oxygen" katika Hospitali ya Mnazi Mmoja.

**MAONI/ USHAURI NA MPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuingizia fedha zilizopangwa kwa Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa wakati, ili kuweza kutuo huduma za matibabu kwa wagonjwa wanaofikishwa katika Hospitali hiyo.

*(b)* Kamati inaiomba Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuendelea kutoa elimu pamoja na kuwashajihisha wanafunzi kusoma masomo ya sayansi, kwa lengo la kupata wataalamu wazawa katika kada tofauti za afya.

*(c)* Aidha, Kamati inaishauri Serikali kuangalia upya suala linalohusiana na maslahi ya wafanyakazi wa kada za afya, kwani wanafanya kazi katika mazingira magumu na hatarishi kwa afya zao. Iwapo maslahi yao yatabaki kama yalivyo sasa, kunapelekea kupunguza morali ya kazi na baadhi yao kuondoka au kuhama na kutafuta kazi katika sekta binafsi.

*(d)* Kamati inaiomba Bohari Kuu ya Dawa Zanzibar kuandaa utaratibu mzuri wa usambazaji wa dawa katika Vituo vyetu vya Afya, Hospitali za Mikoa, Wilaya

na Rufaa, ili kupunguza malalamiko ya ukosefu, uchelewaji na upatikanaji wa dawa katika hospitali zetu.

## C. PROGRAMU YA TIBA

Programu hii ina jukumu la kusimamia utoaji wa huduma katika Vituo vya Afya vya Vijiji, Hospitali za Wilaya na Mikoa. Pia, inahusika na utoaji wa huduma kupitia Mpango wa Damu Salama, Ushauri kwa Hospitali Binafsi, Uchunguzi wa Maradhi na kusimamia uendeshaji wa shughuli za Mabaraza ya Kitaaluma pamoja na Huduma za Mkono kwa Mkono ambapo, huduma hizo zinatolewa kupitia Programu Ndogo ya Huduma za Matibabu na Huduma za Uchunguzi.

### I. PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA ZA MATIBABU

Kamati katika kutekeleza majukumu yake ilibahatika kuzikagua Taasisi mbali mbali ambazo zinatekelezwa kupitia Programu Ndogo hii na kubaini changamoto kadha kama zinavyoonekana katika Ripoti hii.

### TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)

Taasisi ya Utafiti wa Afya Zanzibar (ZAHRI) imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nambari 5 ya Mwaka 2018. Taasisi hii ni miongoni mwa Taasisi muhimu za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa mujibu wa Sheria ya kuanzishwa kwake ambapo imepewa majukumu ya kusimamia upatikanaji wa taarifa za kisayansi kwa ajili ya kuendeleza na kuimarisha njia na mbinu mbali mbali za tiba na udhibiti wa magonjwa ya binaadamu nchini, ili kufikia malengo yaliokusudiwa.

**CHANGAMOTO ZA TAASISI YA UTAFITI WA AFYA ZANZIBAR (ZAHRI)**

Taasisi hii inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Uwepo wa madeni makubwa na ya muda mrefu ya watafiti wa nje wanaofanyakazi za tafiti za afya katika taasisi hii pamoja na Wajumbe wa Bodi.

*(b)* Ukosefu wa usafiri wa kudumu kwa Mkurugenzi wa taasisi pamoja na watendaji.

*(c)* Ukosefu wa maeneo kwa ajili ya kuanzisha shamba darasa la mimea ya tiba asili ambayo inahitajika kufanyiwa utafiti kwa ajili ya matumizi ya binaadamu.

*(d)* Ukosefu wa bajeti ambapo tangu taasisi hii ya afya kuanzishwa haijawahi kuingiziwa fedha kutoka Serikalini, hali inayopelekea watendaji kupoteza morali ya kazi.

*(e)* Ukosefu wa jenereta kwa ajili ya matumizi ya jengo, hali inayopelekea mashine zilizopo kukaa bila ya matumizi yoyote na mwisho kuharibika.

*(f)* Ukosefu wa ajira kwa vijana wa Binguni katika taasisi, ambapo wamejitolea wazee wao maeneo yao kwa ajili ya Taasisi hii ya Serikali.

*(g)* Kukosekana kwa Kitengo cha Uhasibu pamoja na Mkaguzi wa Ndani katika Taasisi hii ya Utafiti wa Afya tangu kuanzishwa kwake.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuitengea bajeti Taasisi ya Utafiti wa Afya, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa wakati na kuweza kupunguza madeni yanayowakabili kwa muda mrefu ya watafiti wa nje pamoja na wajumbe wa Bodi.

*(b)* Kamati inaiomba Taasisi ya Utafiti wa Afya kuandaa utaratibu wa kufanya Tafiti juu ya dawa za tiba asili zinazotumiwa na wakunga wetu wa jadi haswa kwa mama wajawazito wanazozitumia katika kipindi chao cha uzazi.

*(c)* Kamati pia inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji na Mifugo kuwapatia eneo maalum Taasisi ya Utafiti wa Afya kwa ajili ya kuanzisha Shamba Darasa la mimea ya tiba asili kwa ajili ya kuenzi mimea inayotoweka duniani ambayo ni muhimu kwa tiba ya afya kwa binaadamu.

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kuipatia usafiri wa uhakika Taasisi hii, ili iweze kuwasaidia watendaji pamoja na Mkurugenzi kwani ni kitu kisichopendeza kuona Mkuu wa Taasisi hana hata usafiri wa uhakika kufika katika eneo lake la kazi.

*(e)* Kamati inaiomba Serikali kuwatizama kwa jicho la huruma vijana wa Binguni waliojitolea katika hatua mbali mbali za mradi wa ujenzi wa Maabara kwa kuwaajiri hata kwa kazi za huduma ikiwemo, ulinzi na usafi wa majengo, suala hili la kupatiwa ajira kwa vijana wa Binguni ni ahadi na maagizo yaliyotokana na Waheshimiwa Rais wetu wa Awamu ya Saba na ya Nane.

*(f)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuharakisha upatikanaji wa Mhasibu pamoja na Mkaguzi wa Ndani katika Taasisi ya Utafiti wa Afya Binguni, kukosekana kuwepo kwa watendaji hawa ndani ya taasisi yoyote ya Serikali kunapelekea kuzorotesha utendaji wa taasisi husika.

*(g)* Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara husika kufanya ununuzi wa jenereta kwa ajili ya Taasisi ya Utafiti wa Afya Binguni,

ili kuzihami mashine zisiharibike mara kwa mara kutokana na tatizo la kukosekana kwa umeme wa uhakika na kupelekea mazingira magumu ya utendaji kazi kwa watendaji wa taasisi hiyo.

## BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA

Baraza la Wauguzi na Wakunga Zanzibar ni chombo kilichoanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nambari 5 ya Mwaka, 2014. Lengo kuu la kuanzishwa ni kusimamia shughuli zote za Wauguzi na Wakunga pamoja na Vyuo vinavyosomesha fani ya Uuguzi na Ukunga katika Visiwa vya Zanzibar. Ambapo kazi za msingi zinazofanyika ni:-

*(i)* Kufanya usajili wa Wauguzi na Wakunga baada ya kufaulu mafunzo yao;

*(ii)* Kusimamia maadili ya wauguzi na wakunga katika kutoa huduma kwa wananchi pamoja na kutoa miongozo ya maadili kwa wauguzi na wakunga wote wanaofanya kazi Zanzibar; na

*(iii)* Kusimamia ubora wa mafunzo katika vyuo vinavyosomesha fani ya Uuguzi na Ukunga hapa Zanzibar.

## CHANGAMOTO ZA BARAZA LA WAUGUZI NA WAKUNGA

Baraza katika utekelezaji wa majukumu yake linakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Baadhi ya Wauguzi kutoongeza muda wa leseni zao kwa wakati hali inayopelekea kuikosesha mapato Serikali pamoja na kufanya kazi kinyume na taratibu za Sheria.

*(b)* Wakuu wa Wilaya na Halmashauri na Mabaraza ya Mji kutowasilisha malalamiko ya Wauguzi na Wakunga katika Baraza pahala panapohusika, baada yake hupitisha maamuzi, ikiwa ni pamoja na kuwaweka ndani jambo linawachanganya kisaikolojia, ambapo kitendo hicho ni kinyume na taratibu za adhabu za makosa ya kitaaluma.

*(c)* Kutopata mashirikiano ya kutosha kutoka kwa walalamikaji wakati wakutafuta ushahidi wa tuhuma zinazowasilishwa mbele ya Baraza.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaliomba Baraza la Wauguzi na Wakunga kufanya kazi kwa kushirikiana na Baraza la Mabaraza ya Madaktari katika kutoa elimu kwa Wauguzi na Wakunga wetu wanaofanya kazi katika vituo vyetu vya afya kuacha tabia ya kufanya kazi bila ya kuwa na leseni ya kuruhusiwa kutoa huduma hizo kwa wananchi.

*(b)* Kamati pia inazishauri Halmashauri pamoja na Mabaraza ya Mji kutofanya Maamuzi ya kesi yoyote inayohusiana na malalamiko ya wauguzi au wakunga bila ya kukaa pamoja na Baraza linalohusika kisheria kusimamia maadili na pale inapotokezea kosa lolote linalohusu utendaji wa kazi taratibu za kufuatwa zimeelekezwa katika Sheria na Kanuni za Wauguzi na Wakunga.

**BARAZA LA MADAKTARI ZANZIBAR**

Baraza la Madaktari Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria Nam. 12 ya Mwaka 1999 ambapo kazi yake kuu ni kushauriana na Wizara kuhusu mwenendo mzima wa ufanyajikazi wa madaktari. Aidha, katika shughuli zake za uendeshaji, Baraza halina ruzuku yoyote kutoka Serikalini na wala Wizarani hivyo linajitegemea

katika kufanya kazi zake kutokana na fedha zinazokusanywa kutoka kwa Madaktari wanaofanya usajili na kukata leseni.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MADAKTARI ZANZIBAR**

*(a)* Madaktari kuajiriwa kabla ya kufanya usajili.
*(b)* Ofisi ya Baraza ni ndogo kulingana na majukumu yake.
*(c)* Ofisi ya Baraza la Madaktari bado haina usafiri.
*(d)* Mfumo wa Kanzidata (Database) ni mbaya kutokana na ukosefu wa mtaalamu wa IT.
*(e)* Makusanyo yote ya Baraza yanayotokana na Ukataji wa Leseni za Udaktari na Kujisajili yote yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Hazina na hakuna fedha zinazorudi, hali inayopelekea Baraza kushindwa kutekeleza majukumu yake kama yalivyopangwa.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inalipongeza Baraza la Madaktari kwa kutekeleza kazi zake licha ya kukabiliwa na mazingira magumu na kuweza kufanikiwa kufanya baadhi ya kazi ikiwemo ununuzi wa vifaa kwa ajili ya ofisi ya Baraza la Madaktari pamoja na kusajili madaktari wa fani tofauti.
*(b)* Kamati, inaiomba Serikali kulipatia fedha za ‘OC’ Baraza la Madaktari kwa ajili ya kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi, kwani wao ni miongoni mwa Taasisi inayokusanya fedha, lakini hakuna fedha yoyote inayorudi kwa ajili ya shughuli za uendeshaji wa ofisi hali inayowapelekea kushindwa kutekeleza mipango waliyojipangia kwa mwaka wa fedha husika.

*(c)* Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kuangalia upya suala la maslahi ya watendaji wa Afya pamoja na stahiki zao nyengine, ili kuweza kufanya kazi katika mazingira mazuri kwa lengo la kuwajengea uwezo wa kufanya kazi kiuzalendo zaidi katika jamii yao inayowazunguka. Kwani kubaki na maslahi madogo kunapelekea madaktari wengi kuondoka na kwenda kutafuta ajira katika Hospitali za Binafsi na wengine hata kuhama nchi.

*(d)* Pia, Kamati inapendekeza kwamba madaktari wote ni lazima wafuate taratibu za kujisajili na kupatiwa leseni kabla ya kuajiriwa, kwani Kamati imepokea taarifa kuwa katika Hospitali zetu zote za Unguja na Pemba asilimia kubwa ya madaktari wanaotoa huduma hawana leseni wala hawajasajiliwa na Baraza la Madaktari kama takwa la Sheria inavyoelekeza.

*(e)* Kamati, inatoa msisitizo kwa jamii kuwashajihisha wanafunzi kusoma kwa bidii masomo ya sayansi kwa ajili ya kupunguza uhaba wa wataalamu wa sayansi katika masuala ya afya.

*(f)* Kamati pia inaupongeza Uongozi wa Baraza la Madaktari kwa kuona umuhimu wa kuanzisha tawi la Baraza la Madaktari kwa upande wa Pemba, hii itasaidia kusimamia maadili na mwenendo wa Madaktari wetu wanaohudumia wananchi wetu.

## HOSPITALI ZA WILAYA MICHEWENI, WETE, KIVUNGE NA MAKUNDUCHI

Azma na malengo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kujenga Hospitali katika kila Wilaya ni kuwasogezea karibu wananchi wake huduma za afya zilizo bora na salama na kuhakikisha utoaji wa huduma hizo zinapatikana wakati wote zinapohitajika.

**CHANGAMOTO ZA HOSPITALI ZA WILAYA MICHEWENI, WETE, KIVUNGE NA MAKUNDUCHI**

Hospitali hizi kwa pamoja zinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Ukosefu wa Madaktari Bingwa katika Hospitali zote za Wilaya.

*(b)* Ukosefu wa Usafiri kwa watendaji wanaofanya kazi katika hospitali hizo.

*(c)* Kutokuingizwa fedha za 'OC' kwa wakati kwa Hospitali zote za Wilaya. Mfano halisi wa hayo, kwa miezi mitatu kuanzia Oktoba hadi Disemba, 2021:

- Hospitali ya Wilaya ya Micheweni ilipangiwa kupata Jumla ya Shilingi 52,433,500/= lakini fedha iliyopatikana ni shilingi 5,712,240/=;
- Hospitali ya Wilaya Makunduchi nayo ilipangiwa shilingi 42,500,000/- ambapo fedha iliyopatikana ni shilingi 3,000,000/- tu kwa ajili ya utekelezaji wa kazi za miezi mitatu yote.

*(d)* Kutokuwepo kwa Muundo wa Utumishi kwa Hospitali ya Wilaya ya Kivunge.

*(e)* Madeni makubwa ya "Overtime", "On call allowance", "Responsible Allowance" pamoja na "Nursing Allowance" kwa madaktari na wahudumu wa afya katika Hospitali ya Wilaya ya Kivunge.

*(f)* Kutokuwepo kwa huduma za Bima ya Afya katika Hospitali ya Wilaya ya Kivunge.

*(g)* Ukosefu wa vifaa vya Maabara na mashine ya Usingizi katika Hospitali ya Wilaya ya Micheweni na Makunduchi.

*(h)* Upungufu wa dawa na vifaa tiba katika Hospitali zote za Wilaya.

*(i)* Ukosefu wa Uzio katika Hospitali na Nyumba za wafanyakazi kwa Hospitali ya Wilaya Makunduchi.

*(j)* Ufinyu wa eneo la kuhifadhia dawa.

(*k*) Kuharibika mara kwa mara kwa vifaa tiba kutokana kukatika katika kwa umeme katika Hospitali ya Wilaya Wete.

(*l*) Uingiaji wa watu kinyume na utaratibu katika wodi za wagonjwa Hospitali ya Wilaya Micheweni.

(*m*) Ukosefu wa Oksijini katika Hospitali zote za Wilaya kwa Unguja na Pemba.

(*n*) Ukosefu wa Damu Salama wakati mgonjwa anapohitaji kusaidiwa katika Hospitali ya Wilaya Makunduchi.

(*o*) Kuharibika mara kwa mara kwa taa katika Chumba cha Upasuaji kwa Hospitali zote za Wilaya.

(*p*) Uhaba wa vifaa kwa ajili ya watoto wanaozaliwa chini ya miezi 9 (Watoto Njiti).

(*q*) Ucheleweshaji wa upelekaji wa dawa katika Hospitali zote za Wilaya kutoka Bohari Kuu.

(*r*) Kukosekana kwa kipoza hewa katika chumba cha upasuaji katika Hospitali ya Wilaya Micheweni.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(*a*) Kamati, inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuziingizia fedha za ‘OC’ kwa wakati Hospitali zote za Wilaya, kwa lengo la kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi na weledi katika kuwahudumia wananchi wa Taifa hili.

(*b*) Vile vile, Kamati inaishauri Serikali pamoja na Tume ya Utumishi Serikalini kukaa kwa pamoja na kulitafutia ufumbuzi suala zima la uhaba wa wataalamu pamoja na watendaji katika Hospitali zetu za Wilaya.

*(c)* Pia, Kamati inaiomba Serikali kuharakisha upatikanaji wa usafiri wa kudumu kwa watendaji wa Hospitali zote za Wilaya wanaoishi katika maeneo ya mbali na hospitali hizo kwa maana ya kituo cha kazi.

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuandaa mpango madhubuti wa ununuzi wa vifaa tiba ikiwemo "Biochemistry Mashine", "Radiographer Machine", Mashine ya Usingizi, "Incubetor Machine", "Digital X-ray Machine" katika Hospitali zetu za Wilaya, ambapo kukosekana kwa vifaa hivyo kunahatarisha maisha ya binaadamu wanaofika katika hospitali hizo kwa ajili ya kupata huduma.

*(e)* Kamati inaishauri Bohari Kuu ya Dawa kuandaa utaratibu mzuri usambazaji na ufuatiliaji wa dawa katika Hospitali zote za Wilaya, ili kuwaondoshea changamoto za kukosekana dawa katika hospitali hizo.

*(f)* Kamati inaiomba Serikali kuharakisha ujenzi Vituo vya Kuzalisha Oksijini kwa Unguja na Pemba pamoja na ununuzi wa mitambo yake, ili kupunguza na hatimae kuondosha kabisa tatizo hilo.

## KITUO VYA MKONO KWA MKONO HOSPITAL YA MICHEWENI, MAKUNDUCHI PAMOJA NA WETE

Kituo cha Mkono kwa Mkono ni Kituo Maalum kwa ajili ya kuwasaidia wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsi ambao ni wanawake na watoto. Kimuundo Kituo cha Mkono kwa Mkono kipo katika Idara ya Tiba katika Kitengo cha Wagonjwa wa Nje (OPD) hospitali. Kitengo hiki kinafanya kazi kwa mashirikiano ya karibu sana na Maafisa kutoka Ustawi wa Jamii, Jeshi la Polisi, Madaktari wa Hospitali za Serikali pamoja na Shirika la 'Save the Children International'.

Dhumuni kuu la kuanzishwa kwa vituo hivi katika kila Hospitali za Wilaya Unguja na Pemba ni kuwasaidia wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia na pamoja na kutoa huduma kwa usalama na usiri katika sehemu zao na bila ya usumbufu wowote.

Pia, huduma mbali mbali zinatolewa katika vituo vyote ikiwemo huduma ya ushauri nasaha, huduma ya ustawi wa jamii, huduma ya rufaa, huduma za kipolisi pamoja na huduma za kiuchunguzi wa kimatibabu kwa wahanga wa vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, ambapo kwa muda mrefu huduma hizi zilikuwa zikiendelea kutolewa isipokuwa katika mazingira yasiyokuwa Rafiki.

Hata hivyo, mnamo mwaka 2015, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kupitia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wizara iliyokuwa ikishughulikia masuala ya Wanawake na Watoto kwa wakati huo pamoja na Shirika la ‘Save the Children’ ziliamua kwa pamoja kuanzisha vituo hivyo maalum vya Mkono kwa Mkono kwa ajili ya kutolea huduma hizi hospitalini na hatimae sasa vituo hivyo kujengwa katika kila Hospitali za Wilaya na mwaka 2018 zilianza kazi rasmi ya kusikiliza na kupokea malalamiko juu ya kesi zinazohusiana na Ukatili na Udhalilishaji wa Wanawake na Watoto.

## CHANGAMOTO ZA VITUO VYA MKONO KWA MKONO

Katika utekelezaji wa majukumu yake, vituo hivyo vinakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Uchache wa watendaji katika vituo vyote vya Mkono kwa Mkono hususan Maafisa Ustawi wa Jamii.

*(b)* Uchache wa fedha za uendeshaji (OC) ambapo mfano halisi unaonekana katika robo hii ya Oktoba – Disemba, 2021 kwa Kituo cha Mkono kwa Mkono cha Micheweni kuingiziwa fedha 184,000 sawa na asilimia 14.7 ya utekelezaji.

*(c)* Ukosefu wa askari dhamana anayeshughulikia kesi za udhalilisha zinaporipotiwa Vituoni humo.

*(d)* Uelewa mdogo wa wazee juu ya kuziripoti kesi za udhalilishaji wa watoto na ukatili wa kijinsia.

*(e)* Ukosefu wa vitendea kazi katika Vituo vyote ikiwemo Kompyuta za kuhifadhi kumbukumbu pamoja na vifaa vya kuchunguzia wahanga katika hatua ya kwanza.

*(f)* Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri ya utendaji kati ya Polisi, Afisa Ustawi wa Jamii, Watendaji wa DPP na Mahakama juu ya ufuatiliaji wa kesi hizo.

*(g)* Kutokuwepo kwa madawati ya mtoto ya udhalilishaji katika vituo vyote vitatu.

*(h)* Ukosefu wa elimu kwa wahanga wa vitendo vya udhalilishaji hususan Vijijini.

*(i)* Kukosekana kwa kituo cha “One Stop Centre”,

*(j)* Ukosefu wa Mabaraza ya Shehia ya ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji na utakitili wa kijinsia kwa wanawake na watoto.

*(k)* Ucheleweshaji wa usikilizaji wa kesi za udhalilishaji katika Mahakama zetu.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaishauri Serikali na Wizara husika kuandaa mpango Madhubuti wa kuweza kuwaendeleza wahanga wote wanaokumbana na vitendo vya udhalilishaji na ukatili wa kijinsia, ili wasione kuwa jamii na Taifa lao halipo pamoja nao.

*(b)* Kamati inaiomba Serikali kuishirikisha kikamilifu Mamlaka ya Uhujumu Uchumi (ZAECA) katika masuala yanayohusiana na kesi za udhalilishaji.

*(c)* Kamati inaiomba tena Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kuharakisha uanzishaji wa Mabaraza ya Shehia katika kila Shehia yatakayoshughulikia ufuatiliaji wa kesi za vitendo vya udhalilishaji kwa Wanawake na Watoto.

*(d)* Kamati inaishauri Wizara ya Afya kupitia Idara yake ya Tiba kuaanda utaratibu wa utoaji wa huduma za ushauri nasaha katika Skuli pamoja na Madrasa zetu, ambapo Kamati imebaini kukosekana uwepo wa huduma hiyo ndio kunapelekea Watoto wetu kuathirika kisakolojia baada ya kukumbana na udhalilishaji.

*(e)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuandaa somo maalum linalohusiana na udhalilishaji katika mtaala wa Elimu ya Msingi mpaka Sekondari.

*(f)* Kamati pia inaiomba Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kupitia Ofisi ya Mufti kuandaa utaratibu mbadala wa utoaji wa vibali kwa Madrasa, kwani Kamati imegundua kesi za vitendo vya udhalilishaji takriban nyingi zinajitokeza ndani ya Madrasa zetu za vyuo vya Kusomeshea Qur-an.

*(g)* Kamati inaiomba Wizara ya Afya kufanyakazi kwa mashirikiana ya karibu na vyombo vyetu vya Habari vya ndani, Redio na Magazeti kutoa elimu kwa jamii juu ya athari za vitendo hivyo vya udhalilishaji na ukatilia wa kijinsia kwa wanawake na Watoto.

(h) Kamati inaishauri Serikali kuyaimarisha zaidi Mabaraza yetu ya Shehia yanayofuatilia kesi za udhalilishaji katika maeneo yanayowazunguka.

## WARATIBU WA SHEHIA WANAOSHUGHULIKIA MASUALA YA VITENDO VYA UKATILI NA UDHALILISHAJI KWA WANAWAKE NA WATOTO

### Chimbuko la Waratibu wa Shehia wa Masuala ya Ukatili na Udhalilishaji

Wazo la kuwa na Waratibu wa Shehia liliibuka mwaka 2000 kufuatia kujitokeza kwa matukio mbali mbali yanayohusiana na udhalilishaji wa kijinsia, wanawake na watoto ndani ya Shehia zote za Zanzibar. Aidha, kulikuwa na malalamiko mengi kuhusiana na vitendo vya udhalilishaji wa masuala ya kijinsia na watoto katika jamii. Lengo la kuanzishwa Waratibu hawa lilikuwa ni kuratibu na kufuatilia kwa karibu masuala ya udhalilishaji pamoja na kuyalea Mabaraza ya Watoto yaliyoundwa katika Shehia, ili kutanua wigo wa kukabiliana na changamoto mbali mbali za kijinsia na zinazowakabili watoto wa rika tofauti.

Vile vile, katika kukabiliana na changamoto hizo ni pamoja na kuwashirikisha Masheha wa Shehia husika, Maafisa Jinsia na Watoto wa Ngazi za Wilaya na hatimae huwasilishwa katika ngazi ya Wizara kupitia Idara ya Jinsia na Watoto kwa hatua zaidi.

### Kazi za Waratibu

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Waratibu wa Shehia ni pamoja na:

(i) Kutoa elimu kwa jamii katika Vijiji dhidi ya masuala ya Ukatili na Udhalilishaji wa Jinsia;

*(ii)* Kuibua kesi za Udhalilishaji wa Kijinsia na kuzifikisha katika Mamlaka husika, ili kupatiwa ufumbuzi wa kisheria;

*(iii)* Kuelimisha wanawake katika jamii namna ya kufahamu haki zao kisheria na kutoa elimu kwa Mabaraza ya Watoto juu ya Udhalilishaji wa Kijinsia pamoja na kujua haki na wajibu wao.

**Utekelezaji wa Kazi za Waratibu**

Katika kipindi hiki kuanzia Oktoba – Disemba, 2021, Waratibu wa Shehia walifanikiwa kuendeleza majukumu yao kwa kushirikiana na Kamati za Kupinga Masuala ya Udhalilishaji (Gender Based Violence) kwa wanawake na watoto katika shehia zao waliweza kuibua malalamiko 12, Wilaya ya Chake Chake 5, Wilaya ya Wete 3, Wilaya ya Micheweni 2 na Wilaya ya Mkoani 2 ya udhalilishaji wa kijinsia na kufikishwa kwa Maafisa wa Jinsia na Watoto wa Wilaya.

## CHANGAMOTO ZA WARATIBU WA SHEHIA

Waratibu wa Shehia katika kutekeleza majukumu yao wanakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Ukosefu wa posho la usafiri jambo ambalo linapelekea ugumu wa kuvifikia vijiji vilivyomo katika Shehia zao;

*(b)* Ukosefu wa posho la mawasiliano sababu inayowapelekea kushindwa kufuatilia matukio ya kesi za udhalilishaji hata kwa kupiga simu;

*(c)* Rushwa ya Muhali katika jamii;

*(d)* Upatikanaji wa ‘OC’ ndogo hali inayopelekea Waratibu kushindwa kulipwa posho la kazi;

(e) Kuharibiwa kwa ushahidi na baadhi ya watendaji wanaoshughulikia masuala haya ya udhalilishaji ikiwemo Jeshi la Polisi, Madaktari, Waendesha Mashtaka pamoja na Mahakimu wanaoziendesha kesi hizo;

(f) Kukatishwa kwa masomo kwa watoto wanaopatwa na majanga ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia;

(g) Ucheleweshwaji wa usikilizwaji wa kesi zinazohusiana na vitendo vya udhalilishaji;

(h) Kuachiwa huru kwa watuhumiwa baada ya kufikishwa katika vyombo vya vya Kisheria;

(i) Ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu masuala ya vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa watoto waliopo skuli hasa katika Skuli za Maandalizi na Msingi; na

(j) Kuwepo kwa madeni ya muda mrefu kwa Waratibu wa Shehia yanayohusiana na ufuatiliaji wa kesi za udhalilishaji.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

(a) Kamati inaziomba Taasisi zote zinazoshughulikia masuala ya Vitendo vya Udhalilishaji wa Kijinsia kwa watoto na wanawake kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu katika kuhakikisha zinapambana na kutokomeza vitendo hivyo katika jamii zetu.

(b) Kamati inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora kuandaa mpango madhubuti wa kuharakisha usikilizaji wa kesi zinazohusiana na vitendo vya udhalilishaji.

(c) Kamati inaishauri Wizara Afya kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii kuliangalia kwa jicho la huruma suala la ukosefu wa posho la kazi, posho la mawasiliano na posho la usafiri kwa Waratibu wetu wa Shehia wanaoshughulikia Masuala

ya Udhalilishaji katika Shehia zetu, ambapo kwa sasa Mratibu wa Shehia analipwa posho la shilingi 30,000/-.

## BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR

Bohari Kuu ya Dawa inajukumu la kupokea, kuhifadhi na kusambaza dawa, vifaa vya utabibu, reajenti pamoja na vifaa vyengine vya uchunguzi kwenye hospitali na vituo vyote vya afya vya Serikali na baadhi ya vituo vya binafsi Unguja na Pemba. Vile vile, Kamati ilipata taarifa kwamba manunuzi ya dawa yanafanywa na Wizara kupitia Kitengo chake cha Manunuzi (PDMU) kwa kushirikiana na Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali.

## CHANGAMOTO ZA BOHARI KUU YA DAWA ZANZIBAR

Bohari Kuu ya Dawa inakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Upatikanaji mdogo wa dawa na vifaa vya utabibu kutoka MSD pamoja na wasambazaji wengine wenye mikataba na Wizara. Hali hii inapelekea Bohari kushindwa kusambaza dawa za kutosha na hivyo kusababisha baadhi ya huduma muhimu kushindwa kutolewa kwa ufanisi.

*(b)* Uhaba wa wafanyakazi, vitendea kazi na bajeti ndogo ya kuendeshea huduma ni changamoto kubwa kwa Bohari ya Dawa Pemba, ili iweze kutoa huduma za usambazaji wa dawa kwa ufanisi.

*(c)* Kukosekana kwa walinzi kwa ajili ya kulinda eneo la Bohari Pemba. Kwa sasa walinzi wanaotumika ni wa Kampuni ya Ujenzi ambao wataondoka mara tu ujenzi utakapokamilika.

*(d)* Upotoshaji wa taarifa za upatikanaji wa dawa vituoni hasa wakati wa ziara za viongozi wa Serikali. Bohari ya Dawa imebaini kuwa baadhi ya wafanyakazi wa vituo vya afya wanashindwa kutoa huduma kwa visingizio kuwa hawajasambaziwa dawa na vifaa wakati vifaa hivyo vinapatikana kwenye vituo vyao.

*(e)* Uhaba wa fedha za uendeshaji (OC) unaathiri utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Bohari.

*(f)* Kuchelewa kukamilika kwa mchakato wa Bohari kuwa Taasisi inayojitegemea inasababisha Bohari kuendelea kuwa tegemezi na kushindwa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi na kwa wakati.

*(g)* Ukosefu wa usafiri kwa Bohari ya Dawa Pemba kwa ajili ya usambazaji wa dawa katika maeneo yote ya mjini na vijijini, ambapo kwa Pemba gari iliopo ni moja na chakavu sana na ndio inayotumika kusambazia dawa sehemu zote kwa siku, gari hiyo inaweza ikapangiwa usambazaji wa dawa Wilaya zisizopungua nne (4).

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa kukamilisha Mradi wa Ujenzi wa Bohari ya Dawa Pemba katika eneo la Vitongoji, ili kusaidia kupunguza changamoto wa ukosefu wa dawa katika vituo vyetu vya afya pamoja na hospitali zetu zilizopo katika Wilaya na Mikoa.

*(b)* Kamati inaiomba pia Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Bohari Kuu ya Dawa kuandaa mpango wa mafunzo kwa maafisa wote wa Afya wa Wilaya juu ya umuhimu wa ufuatiliaji na usambazaji wa dawa kwa wakati katika vituo vya afya Vijijini.

*(c)* Vile vile Kamati inaiomba Ofisi ya Mfamasia Mkuu wa Serikali pale inapotokezea Wahisani na Wafadhili wa Maendeleo, Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi pamoja na Wabunge wa Majimbo wanapotoa msaada wa vifaa tiba katika vituo vyetu vya afya basi ni vyema kabla ya kukabidhiwa kwa vifaa hivyo katika kituo husika kufanyike ukaguzi wa kina, kwani Kamati katika kutekeleza majukumu yake imebaini vifaa vingi tiba vinavyotolewa kwa njia ya msaada huwa havifai kutumika kwamba ni chakavu au vifaa hivyo vishapitwa na mifumo teknolojia iliopo sasa kimatumizi. Mfano halisi, kuna vifaa vingi vipo katika HospitalI yetu ya Mkoa ya Abdalla Mzee Pemba na Hospitali ya Wilaya Wete havifai, ambapo jamii wakishaona katika T.V na wanapokwenda hospitali kufuata huduma wakiambiwa hazipo ndio malalamiko yanapoanza.

*(d)* Kamati pia inaiomba Serikali kuipa kipaumbele kifedha Bohari Kuu ya Dawa kwani imegundua uingizaji wa fedha na mahitaji yaliopo nchini hayaendani ambapo kwa mwaka 2019/2020 fedha zilizokuwa zikihitaji kwa matumizi ya dawa ilikuwa ni Bilioni 50 ila mpaka mwaka wa fedha ulipomaliza fedha iliopatikana ni Bilioni 8 tu. Aidha, kwa mwaka 2020/2021pia mahitaji ya fedha zilizokuwa zikihitaji katika matumizi ya dawa yalikuwa ni Bilioni 61, lakini mpaka mwaka wa fedha ulipomalizika Bohari haikupatiwa fedha yoyote na kama inavyofahamika bila ya uwepo wa dawa nchini kunahatarisha afya na maisha ya wananchi wetu ambao ndio tegemeo la Taifa hili na kunaipelekea Bohari kukopa na mwisho kushindwa kulipa fedha za “Supplier”.

*(e)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Afya kuandaa kikao cha pamoja baina yao na wazabuni wanaolete dawa nchini, kwani Kamati inayo taarifa kuwa kuna baadhi ya wanaoleta dawa wamesita kutoa huduma za uletaji wa dawa na vifaa tiba kwa Bohari yetu kutokana na madeni makubwa wanayodai bila ya malipo kwa muda mrefu. Mfano halisi wa madeni hayo ni:

| DENI LINALOTOKANA NA DAWA NA VIFAA TIBA | |
|---|---|
| **MZABUNI** | **DAWA ZILIZOPOKELEWA HADI KUFIKIA JULAI 31, 2021** |
| ABBORT | 1,753,500,000 |
| SALAMA PHARMACETICAL LTD | 1, 426,243,338 |
| KAT MED GROUP | 1,436,036,500 |
| WIZARA (NEBULA) | 13,650,000 |
| KAS MAD | 57,710,000 |
| JUMLA | **4,687,139,838** |
| **DENI LINALOTOKANA NA MAKATO YA ZIADA YA KODI YA ONGEZEKO LA THAMANI** | |
| SALAMA PHARMACETICAL LTD | 224,631,290 |
| KAS MAD | 12,606,525 |
| M&D CHEMICAL | 88,764,727 |
| JUMLA | **326,002,542** |
| JUMLA KUU | **5,013,142,380** |

*(f)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Bohari Kuu ya Dawa kuzisimamia na kuzifuatilia kesi zote zinazohusiana na wizi wa dawa kwa baadhi ya watendaji wasio waaminifu katika hospitali pamoja na vituo vyetu vya afya.

## II. PROGRAMU NDOGO YA HUDUMA NA UCHUNGUZI

Ni dhahiri kwamba huduma bora za matibabu zinahitaji uchunguzi sahihi. Kwa kulizingatia hilo, Kamati pia ilizikagua Taasisi hizi na kugundua changamoto mbali mbali wanazokumbana nazo Wakuu wa Taasisi hizo pamoja na watendaji katika kutekeleza majukumu yao.

### WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR

Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi imeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nambari 2 ya Mwaka 2006 na marekebisho yake Sheria Nambari 3 ya Mwaka 2017. Lengo kuu la kuanzishwa kwa Wakala huu ni kusimamia udhibiti wa ubora na usalama wa Chakula, Dawa na Vipodozi vinavyoingia na kutumika ndani ya Zanzibar, Kuimarisha Utawala Bora katika Huduma za Wakala pamoja na Kuimarisha Huduma za Maabara ndani ya Zanzibar.

### CHANGAMOTO ZA WAKALA WA CHAKULA, DAWA NA VIPODOZI ZANZIBAR

Wakala unakabiliwa na changamoto zifuatazo katika utekelezaji wa majukumu yake:

*(a)* Kutofuatwa kwa taratibu za uteketezaji wa dawa, chakula na vifaa kwa baadhi ya taasisi za Serikali na Binafsi;
*(b)* Zuio la Ajira kutoka Serikalini;
*(c)* Uhaba wa wataalamu wa ukaguzi wa mifugo Zanzibar;

*(d)* Ukosefu wa huduma ya maji na umeme katika mradi wa Ujenzi wa Jengo Jipya la Maabara;

*(e)* Ucheleweshaji wa ukamilishaji wa Mradi wa Ujenzi wa Maabara ya Kisasa ya Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi Zanzibar, ambapo mradi ulitakiwa ukamilike kwa mujibu wa mkataba ndani ya miezi 18 tokea ulipoanza utekelezaji wake;

*(f)* Uchelewaji wa malipo kwa Mkandarasi sababu inayopelekea kuzorota kwa kumalizika kwa mradi wakati muafaka;

*(g)* Ongezeko la muda wa kazi za mradi ambapo hadi tarehe 26/01/2022 ongezeko la muda wa kazi ishafanyika zaidi ya mara nne "Extension of Work".

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Tume yake ya Utumishi kuwapatia kibali cha ajira Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi kuweza kuajiri wataalamu wanaohitajika katika nafasi 10 za wataalamu waliostafu.

*(b)* Kamati inaishauri Wizara kwa kushirikiana na Wakala kuandaa utaratibu maalum wa utoaji wa elimu Mjini na Vijijini juu ya athari wa utumiaji bidhaa zisizokaguliwa.

*(c)* Kamati inauomba Wakala kufanya kazi kwa karibu na Taasisi zote zinazohusiana na ukaguzi wa bidhaa na vifaa, ili kusaidia Serikali kuzuia uingizaji wa bidhaa na vifaa visivyo na sifa na tija kwa matumizi ya mwanaadamu na hatimae kuleta athari za kimazingira nchini.

*(d)* Kamati inaishauri Taasisi ya Dawa na Vipodozi Zanzibar (ZFDA) kutoruhusu uingizwaji wa madawa nchini bila ya kufuta utaratibu uliowekwa kisheria wa kupata vibali vya uletaji madawa hali inayopelekea athari kubwa ya uingizwa wa dawa kinyume na utaratibu na yaliopitwa na muda wa matumizi.

*(e)* Kamati inaiomba Serikali kuondoa utitiri wa uchukuaji wa Sampuli na ukaguzi wa bidhaa na mizigo inayoingia nchini hali inayopelekea wafanyabiashara wa ndani na nje kulalamikia huduma zinazotolewa na taasisi za Serikali.

*(f)* Kamati pia inaiomba Serikali kuweka utaratibu mzuri wa ulipaji wa malipo ya Mkandarasi pale tu anapokamilisha kazi, ili kuepusha kutokumalizika kazi kwa wakati na ongezeko la gharama zisizokuwa za lazima.

## WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali inajukumu la kufanya ukaguzi wa udhibiti wa kemikali na uchuguzi wa sampuli mbali mbali zikiwemo za makosa ya jinai (forensic), udhibiti wa kemikali, dawa na chakula kwa ajili ya kulinda afya na usalama wa mtumiaji katika jamii pamoja na mazingira yaliomzunguka.

## CHANGAMOTO ZA WAKALA WA MAABARA YA MKEMIA MKUU WA SERIKALI

Wakala katika utekelezaji wa majukumu yake unakabiliwa na changamoto zifuatazo:-

*(a)* Wakala wa Maabara kuendelea kupokea fedha kidogo za ruzuku ambazo zinapelekea changamoto katika kutekeleza shughuli zao zilizopangwa kwa mujibu wa bajeti hivyo inapelekea kutokutekeleza shughuli zake kwa ufanisi ikiwemo:

- Kukosekana kuwapeleka watumishi katika mafunzo ya kitaalamu, ambayo yangewajengea uwezo wa kiutendaji kwa matumizi ya mashine mpya zilizonunuliwa.

- Kukosekana kufungwa na kutumika kwa mashine ambazo zinahitaji vitendanishi (reagents) muhimu kwa maabara ambazo zina gharama kubwa.

*(b)* Kutokuwepo kwa malipo kwa baadhi ya Taasisi za Serikali zinazopeleka kazi zao kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kufanyiwa kazi, ambapo Jeshi la Polisi linadaiwa na Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali shilingi milioni nane, laki mbili na arubaini elfu (8,240,000/=) katika robo ya nne ya mwaka 2020/2021, katika ya deni hilo jumla ya shilingi milioni tano (5,000,000/=) ni deni linalotokana na huduma za uchunguzi wa vinasaba na jumla ya deni lote ni shilingi milioni mia na thelathini na saba na ishirini na nne elfu (137,024,000/=).

*(c)* Baadhi ya nafasi zinakaimiwa kwa muda mrefu na bila ya uteuzi wowote. Kwa mfano, Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na kurugenzi za ndani, ambapo unakosesha ufanisi wa utekelezaji wa majukumu ya maabara.

*(d)* Uhaba wa wataalamu wabobezi katika maabara.

*(e)* Ufinyu wa bajeti ya uendeshaji wa shughuli za Mkemia Mkuu wa Serikali, hali inayopelekea kuchelewa kutoa majibu ya sampuli zinazowasilishwa kwao kwa ajili ya uchunguzi.

*(f)* Kutokuwepo kwa mashirikiano ya karibu katika Kesi za Udhalilishaji miongoni mwa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka (DPP) na Jeshi la Polisi.

*(g)* Kukosekana kwa sehemu (jengo) la kuweka na kuhifadhia "chemicals" chakavu zilizomo ndani ya nchi.

*(h)* Maslahi madogo kwa watendaji wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali.

*(i)* Kutokuwepo kwa udhibiti imara wa uingizwaji wa kemikali nchini.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inaziomba Taasisi za Serikali ikiwemo Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Jeshi la Polisi, Ofisi ya Muendesha Mashtaka wa Serikali (*DPP*) na Mahkama kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu hususan katika kesi zenye vielelezo vinavyopelekwa kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu kwa ajili ya kufanyiwa uchunguzi, ili kuweza kuwasilishwa Mahkamani kwa ushahidi. Kwani kuchelewa kuwasilishwa kwa vielelezo hivyo kwa wakati hupelekea ushahidi kukataliwa na kesi kufutwa.

*(b)* Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya kutafutwa eneo maalum kwa ajili ya kuangamiza bidhaa na kemikali ambazo zimeshapitwa na muda wa matumizi kwa binaadamu kwa kushirikiana na Mamlaka na Idara ya Mazingira, kwa ajili ya kufanya uangamizaji huo, ili kuepusha athari za kimazingira katika jamii.

*(c)* Kamati inaiomba Serikali kuajiri wataalamu weledi, wazalendo wenye uwezo wa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa, kwa lengo la kuepusha utoaji wa majibu ya sampuli yasiyosahihi kwa vielelezo vinavyowasilishwa kwao kwa ajili ya kufanyiwa kazi.

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kufanya uteuzi wa kujaza nafasi zilizowazi ikiwemo ya Mkurugenzi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali pamoja na kurugenzi nyengine za ndani, ambapo nafasi hizo zinakaimiwa kwa muda mrefu. Hivyo, kubaki kama zilivyo kunapunguza uwezo na kasi ya utendaji wa Wakala huo.

*(e)* Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa mwaka 2022/2023 kutenga fedha kwa ajili ya Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, kwa lengo la kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi zaidi kwa kuepusha kisingizio cha ukosefu wa bajeti.

*(f)* Pia, Kamati inaziomba Taasisi zote zinazopeleka kazi zake kwa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kufanya malipo kwa ajili ya kufanyiwa kazi zao wanazozipeleka za uchunguzi wa sampuli, ili kuusaidia Wakala kuweza kufanya kazi zake kwa ufanisi zaidi.

*(g)* Kamati inauomba Uongozi wa Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali kuendelea kutoa elimu juu ya matumizi ya "chemicals" hatarishi hususani katika Skuli zetu za Sekondari.

*(h)* Kamati inaiomba Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Wakala wa Maabara wa Mkemia Mkuu wa Serikali kuzifuatilia Taasisi zote ikiwemo Jeshi la Polisi wanaodaiwa madeni ya muda mrefu na bila ya kufanya malipo yoyote kuhusiana na kazi hizo.

## KITENGO CHA KUPAMBANA NA UDHIBITI WA MAJANGA YA DHARURA YA KIAFYA ZANZIBAR

Kitengo cha Kupambana na Udhibiti wa Majanga ya Dharura ya Kiafya Zanzibar kina jukumu la kuhakikisha kinajiwekewa tayari, kukabiliana na kudhibiti pamoja kujirudisha katika hali ya kawaida (*recovery*) dhidi ya majanga na dharura za kiafya hapa nchini. Miongoni mwa maandalizi muhimu na ya msingi kabisa ni pamoja na kuweka mpango madhubuti wa upatikanaji wa rasilimali fedha na rasilimali watu, kuandaa miongozo na kutoa mafunzo.

Aidha, hutumika kama kitovu cha kuratibu taarifa, ili kusaidia hatua za kukabiliana na dharura na majanga ya kiafya na kuimarisha mawasiliano kati ya taasisi husika.

**MAFANIKIO YALIYOPATIKANA KWA KUANZISHWA KITUO CHA KUPAMBANA NA UDHIBITI WA MAJANGA YA DHARURA YA KIAFYA ZANZIBAR**

*(i)* Kuwepo upatikanaji wa uhakika wa rasilimali fedha na kuhakikisha chanjo inawafikia walengwa kwa wakati na inatolewa katika viwango vinavyokubalika kimataifa.

*(ii)* Kufanyika kwa mafunzo kwa wafanyakazi wa kada za Afya 102 kutoka hospitali za Unguja na Pemba zikiwemo hospitali binafsi. Mafunzo hayo yalilenga kuwafundisha watoa huduma za afya matumizi sahihi ya oksijini, ili waweze kutoa huduma bora na zenye ufanisi kwa wagonjwa wa UVIKO – 19 na wengine wenye shida ya mfumo wa hewa pamoja na wenye kuhitaji huduma za uangalizi maalum. Aidha, mafunzo hayo pia yalielekeza jinsi ya utaratibu mzima wa kumfanyia mgonjwa tathmini, ili kuweza kumpatia tiba sahihi. Watalaamu waliopatiwa mafunzo hayo walikuwa 20, wakiwa 10 kutoka Unguja na 10 kutoka Pemba.

*(iii)* Kuanzishwa kwa utoaji wa huduma za upimaji wa UVIKO – 19 imesaidia kuongeza mapato ya Wizara ya Afya na Serikali kwa ujumla.

Kuanzia mwezi wa Juni hadi Septemba, 2021 jumla ya watu 56,248 wamechanjwa kama inavyoonekana katika jadweli hapo chini.

| | **AINA YA CHANJO** | **IDADI YA WALIOCHANJWA** |
|---|---|---|
| 1. | Johson&Johson | 27,204 |
| 2. | Sinovac | 17,806 |
| 3. | Sputnik | 11,238 |
| | **JUMLA** | **56,248** |

## CHANGAMOTO ZA KITENGO CHA KUPAMBANA NA UDHIBITI WA MAJANGA YA DHARURA YA KIAFYA ZANZIBAR

*(i)* Ukosefu wa nyenzo, vifaa pamoja na vitendeakazi vya kisasa kwa tika utoaji wa huduma za afya.

*(ii)* Mwamko mdogo wa wananchi juu ya chanjo ya UVIKO – 19 vijijini.

*(iii)* Kuwepo kwa uvumi juu ya usalama na ubora wa chanjo.

*(iv)* Mashirikiano madogo kwenye baadhi ya taasisi hasa za vikosi vya Ulinzi na Usalama.

*(v)* Ufinyu wa eneo linalotumika kwa ofisi, upimaji wa maradhi pamoja na utoaji wa chanjo.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

*(a)* Kamati, inaipongeza Serikali pamoja na watendaji wa Kitengo cha Kukabiliana na Udhibiti wa Majanga ya Dharura ya Kiafya kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa pamoja na kuwa wazalendo kwa Taifa lao licha ya kukabiliwa na mazingira magumu katika kutekeleza majukumu yao.

*(b)* Aidha, Kamati imefurahishwa na ukusanyaji wa fedha shilingi bilioni 13 kwa muda wa Julai hadi Septemba, 2021 kutokana na masuala ya Kupima Maradhi ya UVIKO - 19. Licha ya kwamba maradhi ni majanga lakini pia huwa na faida na hasara, kwa hapa tunakipongeza Kitengo chetu hichi kwa kufanya kazi nzuri kwa kipindi kifupi.

*(c)* Kamati inashauri Wizara Afya kuzidisha mashirikiano na viongozi mbali mbali wakiwemo Masheha, Madiwani, Wawakilishi, Wabunge, Taasisi za Dini, Mashirika pamoja na Jamii kwa kazi ya utoaji wa elimu na uhamasishaji jamii kuhusiana na njia mbadala za kujikinga na maradhi ya UVIKO-19 (COVID-19) pamoja na upigaji wa chanjo.

*(d)* Vile vile, Kamati inapendekeza kwa Serikali kukipatia fedha Kitengo cha Kukabiliana na Udhibiti wa Majanga ya Dharura ya Kiafya kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi ikiwemo fedha za 'OC', fedha za ununuzi wa mitambo mengine kwa ajili ya kupimia maradhi ya UVIKO – 19.

*(e)* Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kukitafutia eneo la kutosha lenye mazingira rafiki Kitengo cha Kukabiliana na Udhibiti wa Majanga ya Dharura ya Kiafya kwa ajili ya kuweza kufanya kazi zao kwa ufanisi na weledi.

## D. PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA

Programu hii inahusika na masuala ya Uendeshaji na Uratibu wa Wizara kwa Unguja na Pemba ambapo Wizara inaendelea na jukumu la kuimarisha Taasisi zake kwa kuongeza rasilimali watu wanaohitajika katika Taasisi hizo.

## MAFANIKIO YA PROGRAMU

Licha ya mafanikio mbali mbali yaliyopatikaa katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara, lakini pia kuna changamoto ambazo zinaendelea kufanyiwa kazi ikiwemo kupeleka masomoni wafanyakazi wa kada zilizopewa kipumbele kwa mujibu wa mahitaji yaliopo nchini, kutayarisha mpango wa ufuatiliaji na tathmini wa mpango mkakati wa afya, kuimarisha mifumo ya taarifa pamoja na kuratibu shughuli za uandaaji wa Sera, Mipango, Tafiti na Taarifa mbali mbali za Wizara.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA UENDESHAJI NA URATIBU WA WIZARA**

*(a)* Uhaba wa rasilimali watu katika Vituo vyote vya Afya kwa Unguja na Pemba katika ngazi ya Wilaya, Mkoa pamoja na Rufaa. Hili lilibainika katika ziara za ukaguzi wa Kamati ya Ustawi wa Jamii katika Vituo vyote vya Afya walivyokutana navyo lalamiko kubwa walilokumbana nalo ni uhaba wa rasilimali watu, hali inayowapelekea ugumu katika utekelezaji wa majukumu yao ambapo mfanyakazi mmoja kufanya kazi zaidi ya masaa 14 ya kazi.

*(b)* Ukosefu wa Madaktari bingwa wa fani mbali mbali ikiwemo “Radiograhger”, Daktari wa Usingizi, Daktari wa matibabu ya akili na wengineo katika hospitali zetu ikiwemo Abdalla Mzee Hospitali, Hospitali ya Wete, Hospitali Micheweni, Hospitali ya Chake Chake, Hospital ya Kivunge na Hospitali ya Makunduchi.

*(c)* Kutofanyika kwa upembuzi yakinifu katika maeneo yanayojengwa miradi ya ujenzi wa Hospitali zetu, hili Kamati imeliona katika Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Chake Chake. Mradi ambao hadi sasa unaendelea kuutia hasara kubwa Serikali na hata ukikamilika changamoto hizo zitaendelea kuwepo kwa mujibu wa maelezo waliopatiwa Kamati katika ziara za utekelezaji.

*(d)* Ukosefu wa vitendea kazi pamoja na vifaa tiba katika Hospitali zetu zote kwa Unguja na Pemba.

*(e)* Ucheleweshaji wa uingizaji wa OC katika Hospitali za Pemba pia hili Kamati imejionea mwenyewe kuwa katika Hospitali hizo utekelezaji wa kazi ni wa kusuasua. Kwa Mfano, Hospitali ya Micheweni Robo hii ya Oktoba – Disemba, 2021 imeingiziwa Shilingi Milioni 5,712,240, Hospitali ya Wete imeingiziwa Shilingi Milioni 3,000,000.

*(f)* Kutokuwepo kwa mfumo mzuri wa usambazaji Dawa hospitalini, ambapo Kamati ilipopita katika Vituo na Hospitali zote zinakumbana na changamoto ya uhaba wa dawa.

*(g)* Maslahi madogo kwa Madaktari na watendaji wa afya hali inayowapelekea wafanyakazi kuvunjika moyo na kufanya kazi bila ya kuwa na morali ya kazi na mwengine hata kuchukua maamuzi ya kuhama na kwenda kutafuta ajira katika hospitali za binafsi.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kufuatilia kwa karibu Vituo vya Binafsi vya Kulelea Watoto kwa lengo la kufahamu hali halisi ya uendeshaji wa vituo hivyo kuhusiana na fedha wanazopata kutoka kwa Wahisani pamoja na kupiga vita vitendo vya udhalilishaji wa watoto kwenye vituo hivyo, ili watoto waishi katika mazingira ya salama na amani.

*(b)* Kamati, inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuzifanya Hospitali za Wilaya kuwa ni kimbilio la wananchi wetu kwa hatua ya mwanzo kwa kupata huduma za matibabu kabla ya kuelekea Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja. Katika hali hiyo, ni vyema kuboreshwa kwa huduma zinazotolewa kwenye Hospitali hizo za Wilaya, kwa maana ya vitendeakazi ikiwemo vifaa, wafanyakazi pamoja na mambo mengine. Katika hatua hiyo, Kamati inatoa wito kwa jamii kuwa na utamaduni wa kuzitumia Hospitali za Wilaya kwa matibabu ya mwanzo sio kukimbilia moja kwa moja Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na kupelekea msongamano kwa wagonjwa na kusababisha kuchelewa kupata huduma pamoja na usumbufu.

*(c)* Kamati, inaiomba Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuhusu utaratibu wa kufuatwa kwa Miongozo kwa ajili ya wadau pamoja na wahisani mbali mbali wanaotaka kutoa misaada ya vitu tofauti kwenye Vituo vya Afya pamoja na Hospitali zetu ikiwemo dawa na vifaa tiba na nyengine, hivyo ni vyema dawa au vifaa tiba hivyo vifanyiwe uchunguzi na kuthibitishwa ubora wake pamoja na muda wa matumizi, kwa ajili ya kulinda afya za wananchi wetu kwa ujumla.

*(d)* Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto pamoja na taasisi zake zote kuwa makini katika masuala ya afya ikiwemo masuala ya vipimo, chanjo, dawa, ushauri nasaha pamoja na huduma nyengine zinazotolewa katika sekta ya afya, kwani wao wanashughulikia maisha au afya za wananchi, hivyo ni lazima kuwa makini.

*(e)* Kamati, inaushauri Uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuzidisha mashirikiano na watendaji wa wizara, kwa kufanya vikao na ziara za mara kwa mara kwa lengo la kuweza kutatua matatizo yanayowakabili watendaji wao kupitia hospitali, vituo vya afya pamoja na watendaji wengine mbali mbali wa idara, taasisi na vitengo vya wizara ili kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi.

*(f)* Kamati, inaiomba Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia Kitengo cha Malaria kuwaajiri watendaji ambao waliokuwa wakifanya kazi kwa mkataba kwa muda mrefu tokea mwaka 2008 hadi sasa bado hawajaajiriwa, ambao ni watendaji muhimu kwa kitengo hicho.

*(g)* Kamati, inaishauri Serikali kwamba Kamati iliyoundwa ya Kushughulikia Masuala ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji Wanawake na Watoto ambayo ilishirikisha Wizara, taasisi pamoja vitengo tofauti vya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano ikiwemo Jeshi la Polisi, Mahkama, Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka, *ZAECA* pamoja na nyengine

kufanya kazi kwa karibu zaidi kwa lengo la kuvitokomeza kabisa vitendo vya udhalilishaji.

*(h)* Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kupitia Uongozi wa Hospitali ya Wete kuwa wabunifu kwa kuangalia jambo la muhimu zaidi na kulifanyia kazi, kwa ajili ya kuweza kurahisha utekelezaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mfano, suala la tatizo la kukatika kwa umeme ni vyema mitambo au mashine muhimu kuwekewa "*stabilizer"* na kuepusha tatizo la kuungua au kuharibika kwa mashine ama mitambo kwenye Hospitali hiyo.

*(i)* Kamati inaiomba Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuzitafutia ufumbuzi changamoto hizo zinazoikabili Nyumba ya Wazee Limbani ikiwemo suala la daktari, usafiri pamoja na uzio, kwa lengo la kuwaondoshea usumbufu wazee hao na kufaidi vizuri zaidi matunda ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuanzisha Makaazi ya Wazee.

*(j)* Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuwaongezea idadi ya watendaji pamoja na vifaa ambavyo Bohari ya Dawa Pemba inahitaji, kwa ajili ya kuweza kutoa huduma za bohari kwa ufanisi zaidi.

*(k)* Kamati inauomba Uongozi wa Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kutumia Wakala wa Ulinzi JKU kwa kulinda Bohari ya Dawa Unguja na Pemba, kwani fedha nyingi zimetumika katika ujenzi, vifaa pamoja na dawa na vifaa tiba vilivyomo ndani ya bohari.

*(l)* Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kutafutwa eneo au jengo maalum kwa ajili ya kuangamiza bidhaa au chemicals ambazo zimemaliza muda wa matumizi kwa kushirikiana na Taasisi ya Mazingira, kwa ajili ya kuweza kutunza mazingira ya jamii na taifa kwa jumla.

*(m)* Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuwapatia mafunzo watendaji au Maafisa wa Wilaya kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, kwa lengo la kutoa huduma kwa wakati na kuepusha matatizo ya kumaliza dawa au vifaa tiba katika Vituo vya Afya au Hospitali bila ya kupelekwa nyengine au vyengine, ili wananchi waweze kupata huduma wakati wote.

## 3. WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA MAFUNZO YA AMALI

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Mafunzo ya Amali inaundwa na Idara Saba (7), Mabaraza Matatu (3), Bodi Tano (5) pamoja na Ofisi mbili (2) kama ifuatavyo:-

### IDARA

*(i)* Idara ya Uendeshaji na Utumishi;
*(ii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti;
*(iii)* Idara ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
*(iv)* Idara ya Elimu ya Sekondari;
*(v)* Idara ya Elimu Mbadala na Watu Wazima;
*(vi)* Idara ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano katika Elimu;
*(vii)* Idara ya Michezo na Utamaduni katika Elimu; na
*(viii)* Ofisi Kuu Pemba.

### MABARAZA NA BODI

*(i)* Baraza la Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia;
*(ii)* Baraza la Mitihani Zanzibar;
*(iii)* Baraza la Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar
*(iv)* Bodi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali;
*(v)* Bodi ya Taasisi ya Elimu Zanzibar;
*(vi)* Bodi ya Huduma za Maktaba;
*(vii)* Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu; na
*(viii)* Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Elimu.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali ina Programu Kuu Sita (6) ambazo ni hizi zifuatazo:-

*(i)* Programu ya Elimu ya Maandalizi na Msingi;
*(ii)* Programu ya Elimu ya Sekondari;
*(iii)* Programu ya Elimu ya Juu;
*(iv)* Programu ya Elimu Mbadala na Mafunzo ya Amali;
*(v)* Programu ya Ubora wa Elimu; na
*(vi)* Programu ya Utawala na Uongozi.

Programu hizi za Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali zinatekelezwa kwa mashirikiano makubwa ya utatu, yaani baina ya Serikali, wananchi, washirika tofauti wa maendeleo wa ndani na nje.

Pamoja na Programu hizo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pia kuna Miradi Mitano (5), ambayo ni hii ifuatayo:-

*(i)* Uimarishaji wa Elimu ya Maandalizi;
*(ii)* Uimarishaji wa Elimu ya Msingi;
*(iii)* Uimarishaji wa Elimu ya Lazima;
*(iv)* Uimarishaji wa Elimu Mbadala na Amali; na
*(v)* Uimarishaji wa Miundombinu katika Elimu.

## A. PROGRAMU YA ELIMU YA JUU

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo moja ya Elimu ya Juu yenye madhumuni ya kutoa Elimu ya Juu, Ushauri na Utafiti itakayomuwezesha

muhitimu kuweza kujiajiri au kuajiriwa. Sambamba na na hilo, Elimu ya Juu jukumu la kusimamia utoaji wa Elimu Vyuoni na Kazini.

## CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)

Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) ni Chuo Kikuu pekee cha Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Chuo kilianzishwa chini ya Sheria Nam. 8 ya mwaka 1999 sambamba na marekebisho ya Sheria ya Chuo, Nam. 11 ya mwaka 2009. Aidha, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha Sheria ya Mabadiliko ya Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 2016, ambapo Sheria hiyo ilifuta Sheria zilizoanzisha Chuo cha Uongozi wa Fedha - Chwaka (ZIFA), Chuo cha Taaluma za Afya - Mbweni na Taasisi ya Maendeleo ya Utalii - Maruhubi (ZIToD).

Vile vile, kuanzia mwaka wa fedha 2019/2020 Serikali iliridhia kuunganisha Taasisi ya Chuo cha Teknolojia ya Kilimo - Kizimbani (KATI) kuwa sehemu ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar na kuwa Skuli ya Kilimo ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar. Sambamba na hilo, katika mwaka huo huo wa fedha 2019/2020 Serikali pia ilianzisha Skuli Mpya ya Utibabu wa Meno ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar.

Katika mwaka wa fedha 2020/2021, Chuo kimeanzisha Skuli Mpya ya Kompyuta, Mawasiliano na Taaluma za Habari, Skuli hii inatokana na kuunganishwa kilichokuwa Chuo cha Uandishi wa Habari Zanzibar na kuwa sehemu ya SUZA mwaka 2020, ambapo mabadiliko hayo yamapelekea ukuaji mkubwa wa Chuo.

**CHANGAMOTO ZA CHUO KIKUU CHA TAIFA ZANZIBAR (SUZA)**

*(a)* Ufinyu wa miundombinu ya kufundishia yenye kukidhi viwango vya Vyuo Vikuu karibu Kampasi zote za Chuo kulinganisha na mahitaji halisi.

*(b)* Upungufu wa wahadhiri wa ngazi zote hali inayopelekea Chuo kutegemea zaidi walimu wa muda (part – timers) ambapo na hupelekea Chuo kuingia katika madeni makubwa ya malipo ya walimu hao.

*(c)* Uchache wa nafasi na vifaa kwenye maabara za kompyuta.

*(d)* Uhitaji mkubwa wa ukarabati wa miundombinu kutokana na uchakavu wa majengo, ambapo Kamati hii wakati ilipokuwa ikipokea taarifa ya utekelezaji wa robo ya pili ya mwaka wa fedha 2021/2022 iligundua kwamba ukumbi wa Dkt. Ali Mohamed Shein Tunguu tu kila mwaka unatumia Milioni 50,000,000 kwa ajili ya ukaratibu wa jengo kila ifikapo kufanyika kwa mahafali ya Chuo. Hii inatokana na changamoto ya paa lote kuvuja, madirisha pia kupitisha maji na Kamati ilipokwenda ndani zaidi ikabaini kuwa ujenzi huu kikweli haukukidhi viwango. Sambamba na hilo, Kamati pia imebaini Eneo Jipya lilojengwa la IT ndani ya Chuo hiki pia linavuja.

*(e)* Shughuli nyingi zilizopangwa kutekelezwa hasa Makao Makuu ya Chuo bado hazijatekelezwa sababu kubwa ni kutokupatikana kwa fedha ya kutekeleza shughuli hizo, hii inatokana na fedha yote inayokusanya na Chuo kupitia vyanzo vyao vya ndani zote kwenda Mfuko Mkuu wa Hazina na hatimae hata wakiomba fedha hazipatikani hiki ndio chanzo kikubwa kinachokwamisha na kuzorotesha Chuo kisisonge mbele kimaendeleo.

*(f)* Mzigo mkubwa wa madeni yanayoendelea kulipwa kutoka kwa watoa huduma pamoja na wafanyakazi wa ndani. Hali hii hupelekea kutumika kiasi kikubwa cha bajeti kulipia madeni makubwa ya utekelezaji wa kazi zilizopita ambayo Chuo kimekuwa kikilipa tangu mwaka 2019, ambapo Deni lililokuwa likidaiwa

Chuo ni Bilioni 2.5 na hadi kufikia 2021/2022 deni limefika zaidi ya Bilioni 3 ambapo madeni haya yanatokana na walimu wa muda (part timers), deni la ujenzi wa Dakhalia na Nyumba za Walimu Chuo cha Chwaka, Ununuzi wa Kompyuta, madeni ya watendaji ya ‘Over time’, likizo pamoja  na fedha za ufiwa. Sambamba na hilo, Deni la ZSSF tu kwa ujenzi wa dakhalia za wanafunzi Chuo cha Chwaka pamoja na deni la ujenzi wa nyumba za walimu mpaka kufikia June, 2020 limebakia **838,657,640,41/=**. Yote haya yanapelekea mzigo mkubwa kwa Chuo na hatimae kuzorotesha shughuli za utendaji wa Chuo.

*(g)* Ukosefu wa Walimu waliobombea katika fani wanazotoa katika Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA).

*(h)* Uvamizi wa eneo la Razaba liliopo Bagamoyo Tanzania Bara kwa makaazi ya watu, wananchi kulitumia eneo hili kwa kukata miti kinyume na taratibu na pia kuna baadhi ya eneo hili lilo katika miliki ya Chuo Cha Kilimo Kizimbani limeshavamiwa na mwekezaji.

*(i)* Kutokuwepo kwa makabidhiano yoyote ya Vyuo vyote vilivyopelekwa kwa mujibu wa Sheria kuwa chini ya Uendeshaji wa Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) hali inayopelekea Kamati inapohitaji taarifa zake hazipatikani mpaka wapatikane wahusika wenyewe.

*(j)* Uchakavu wa Dakhali za wanafunzi katika Vyuo vyote ikiwemo Chuo cha Fedha – Chwaka, Chuo Cha Afya – Mbweni, Chuo cha Kilimo – Kizimbani, Chuo cha Utalii – Maruhubi na Chuo cha Habari – sababu inayowapelekea wanafunzi kukodi nyumba za watu binafsi nje ya maeneo ya Chuo.

*(k)* Chuo kufuata Muundo wa Utumishi wa Umma hii ni miongoni mwa changamoto kubwa inayopelekea walimu wengi kuondoka kutokana na maslahi madogo wanayolipwa ukilinganisha na Vyuo vyengine nchini hali

inayopelekea Vyuo vyetu kukosa wataalamu wabombezi katika fani zinazotolewa ndani ya Chuo hicho.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA) kuandaa mpango madhubuti wa kuvihami Vyuo vyetu vya ndani kwa kupotea muelekeo na azma ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuvianzisha kwake kwa maslahi ya wananchi wetu na Taifa kwa ujumla.

*(b)* Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Mheshimiwa Waziri wake kuchukua juhudi za makusudi kuliwasilisha suala linalohusiana na changamoto ya ukosefu wa walimu katika Vyuo vyetu yote vya Zanzibar kwa Mheshimiwa Rais, ili kupata ridhaa na kibali cha dharura cha ajira ili kuweza kukihamia Chuo na madeni yasioyalazima yanayotokana na walimu wa muda.

*(c)* Kamati pia inaiomba Wizara kwa kushirikiana na Uongozi wa Chuo Kikuu Cha SUZA kukaa na Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kwa ajili ya kulitafuta njia sahihi ya kukisaidia Chuo kuweza kuyalipa madeni yanayokabiliana nayo hali inayokipelekea hata asilimia ya utekelezaji kushuka siku hadi siku.

*(d)* Kamati pia inaiomba Serikali kwamba Chuo Kikuu cha Taifa (SUZA) baada ya makusanyo yote kupatikana ni vyema wakawarudisha vile Vyuo zinavyokusanya kupitia vyanzo vyao vya ndani wakati fedha hizo zote zinaingia katika "Account" ya SUZA, ili kuweza kuwasaidia kutatua changamoto ndogo ndogo zinazodhorotesha uendeshaji wa Vyuo hivyo ikiwemo Chuo cha Fedha – Chwaka, Chuo Cha Afya – Mbweni, Chuo cha

Kilimo – Kizimbani, Chuo cha Utalii – Maruhubi, Chuo cha Habari – na Chuo cha Biashara – Mombasa.

*(e)* Kamati inaendelea kuishauri Serikali pamoja na Wizara husika pale inapotokezea miradi ya Ujenzi ni vyema kuwashirikisha wataalamu wetu wa ndani pamoja na Wakala wa Majengo ya Serikali (ZBA), ili kuondokana na kasoro za baadae kama ilivyo sasa kwa Ukumbi wa Dr. Ali Mohammed Shein uliopo Tunguu na Eneo la Kompyuta liliopo ndani ya Chuo ambapo linavuja kabla hata hawajafanya makabidhiano ya mwisho.

## TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA

Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia (Karume Institute of Science and Technology – KIST) hapo awali ikijulikana kama Chuo cha Ufundi (Karume Technical College – KTC) ni moja kati ya matunda ya miaka kumi ya mwanzo ya Mapinduzi ya Zanzibar. KIST ni Taasisi inayojitegemea kiutendaji chini ya mwamvuli wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambayo imeanzishwa chini ya Sheria Namba 2 ya Mwaka 2009 ya Baraza la Wawakilishi Zanzibar.

Aidha, 2002 Chuo cha Ufundi Karume ambacho kwa sasa kinajulikana kama Taasisi ya Karume ya Sayansi na Teknolojia kilipata usajili wa kudumu kutoka Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi ambapo sasa kina uwezo wa kutoa mafunzo ngazi ya stashahada katika madaraja ya Cheti na Diploma Chuo kinatoa mafunzo katika fani kumi na mbili (12) ambazo ni:

*(i)* ‘Mechanical’;
*(ii)* ‘Automative’;
*(iii)* ‘Aircraft Maintanence’;

*(iv)* 'Mechanical with Oil and Gas';
*(v)* 'Electrical';
*(vi)* 'Electronic with Renewable Energy';
*(vii)* 'Electronics and Telecommunications';
*(viii)* 'Computer';
*(ix)* 'Civil and Transportation';
*(x)* 'Laboratory Science Technology';
*(xi)* 'Primary Math and Science Teacher'; na
*(xii)* 'ICT with Business'.

Kwa upande wa Shahada, Chuo mpaka kinatoa mafunzo katika fani 3 kama ifuatavyo:-

*(i)* Aircraft Maintenance Engineering;
*(ii)* Civil Engineering; and
*(iii)* Electrical and Electronic Engineering.

**LENGO KUU LA KUANZISHWA KWA TAASISI**

Lengo Kuu la kuanzishwa kwa Taasisi ya Karume ni kutayarisha Vijana kwa kuwapatia mafunzo ya elimu ya ufundi, mafunzo ambayo yatawaweka katika nafasi nzuri ya kuajiriwa na kujiajiri katika Sekta za Umma, Binafsi au kujiajiri wenyewe na kuweza kuongeza kipato chao binafsi na pia Pato la Taifa kutokana na huduma watakazozitoa.

**CHANGAMOTO ZA TAASISI YA KARUME YA SAYANSI NA TEKNOLOJIA**

*(a)* Pamoja na Taasisi kuanza kupata Wakufunzi wenye Shahada ya Tatu, bado idadi yao sio kubwa hasa baada ya kuanza mafunzo ya ngazi ya Shahada. Hii inatokana na kukosa kifungu au ufadhili wa mpango wa kuwasomesha Wakufunzi wake. Hata hivyo, Taasisi inao mpango wa kuwataka Wakufunzi wenyewe kutafuta Vyuo na kusoma kwa mujibu wa fani za Taasisi na kuwaombea mikopo ili kunyanyua hadhi ya Taasisi.

*(b)* Suala la Maslahi ya Watumishi (Mishahara) kubaki kwa kiwango kile kile hata baada ya Taasisi kuanza rasmi kutoa mafunzo ya Shahada ya Kwanza, hali hii ina athari kubwa kwani inaweza kuwafanya wakufunzi waliopo kuondoka, ili kufuata maslahi mazuri sehemu nyengine na kutowavutia wengine kujiunga na Chuo hiki hasa wale wenye Shahada za juu. Kwa upande wa Taasisi imechukua juhudi za kuliwasilisha suala hili katika ngazi za Wizara, ili lifikishwe rasmi Serikalini lakini bado hakujawa na majibu muafaka yaliopatikana.

*(c)* Taasisi pia ina ukosefu wa wafadhili watakaowekeza kwenye miradi mikubwa, ili kuisaidia Taasisi iweze kujiendeleza kwa kujitegemea hali inayopelekea Taasisi hii kuzorota katika utekelezaji wa majukumu wanaojipangia kutokana na utaratibu wa uingizaji OC kutoka Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango bado haupo vizuri.

*(d)* Ukosefu wa bwalo la kufanyia mitihani hii inapelekea kuongezeka kwa udanganyifu wakati wa ufanyaji wa mitihani.

*(e)* Ukosefu wa nyumba za walimu na wafanyakazi.

*(f)* Kutokana na ongezeko la wanafunzi ndani ya Chuo hiki kumejitokeza uhaba wa makaazi kwa wanafunzi wanaotaka kuishi katika dakhalia, ambapo

hupelekea wanafunzi kukodi nyumba za watu binafsi nje ya Chuo na wengine kuanza kujiingiza katika vitendo viovu.

*(g)* Ukosefu wa usafiri wa uhakika kwa watendaji pamoja na wanafunzi wa Chuo.

*(h)* Wanafunzi wa Shahada ya Kwanza kukabiliwa na madeni ya ada, kutokana na kupatiwa asilimia ndogo ya mkopo wanaoupata kutoka katika Bodi ya Mkopo ya Elimu ya Juu Tanzania Bara. Hii inawakabili haswa wanafunzi wetu wanaojiunga na 'Course za Air Craft' kutokana na kutolipiwa kama Course nyengine inawapeleke wanafunzi waliokuwa washaanza kushindwa kuendelea na masomo yao au kubadilisha 'Course'.

*(i)* Ukosefu wa muundo unaoendana na matakwa ya Sheria ya Vyuo Tanzania ambapo Taasisi hii imetakiwa sasa ikakae na watu wa Utumishi wa Umma na kuandaa muundo mpya kwa mujibu wa matakwa ya Sheria ya Utumishi wa Umma Namba 2 ya Mwaka 2011. Kamati inaona kufanya hivyo ni kwenda kinyume na matakwa ya taratibu, miongozo na Kanuni za Vyuo Vikuu hapa Nchini.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kwa kushirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulitafutia ufumbuzi wa haraka suala la maslahi madogo kwa wakufunzi wetu wa ndani kutofanya hivyo ni kunaweza kuwapa nafasi ya kuondoka Serikalini na kwenda kujiajiri katika Vyuo Binafsi.

*(b)* Kamati inaishauri Serikali katika bajeti inayofuata kuiongezea bajeti Taasisi ya Sayansi ya Karume, kwani Chuo hiki kinashindwa kujiendeleza katika ushindani wa kibiashara wa Vyuo Vikuu kutokana na uhaba wa fedha wanazoingiziwa kwa kila robo mwaka.

*(c)* Vile, vile, Kamati inaiomba Taasisi ya Sanyasi ya Karume kwa kushirikiana na Wizara yao kuandaa mpango Madhubuti wa kukitangaza Chuo hili ndani na nje kwa ajili ya kuwavutia wakufunzi pamoja na watu binafsi kuja kuijunga na Taasisi hii.

*(d)* Kamati inaishauri Serikali kwa kushirikiana Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kufanya kikao na Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Tanzania, ili kulipatia ufumbuzi suala la utoaji wa ada ndogo kwa Kada ya "Air Craft", kwani suala hili tayari Kamati ilichukua juhudi ya kulifuatilia pamoja kuliwasisha kwao kwa ajili ya hatua za utatuzi, lakini hadi sasa hakuna mabadiliko yoyote yaliyofanyika baada ya mazungumzo hayo. Ripoti ya Kamati.

*(e)* Kamati inaishauri Taasisi ya Sayansi ya Karume kufanya kazi kwa mashirikiano ya karibu na Vyuo vinavyotoa fani zinazofanana na hizi Tanzania Bara kwa ajili ya kujenga mahusiano ya kubadilishana utaalamu na ujuzi katika kada tofauti za ukufunzi.

## B. PROGRAMU YA UBORA WA ELIMU

Kuanzishwa kwa Programu hii ni kutoa Elimu Bora na sio Bora Elimu katika ngazi zote za Elimu ambapo utekelezaji wake unatekelezwa kupitia huduma mbali mbali ikiwemo Huduma ya Mitaala na Vifaa vya Ufundishaji, Huduma ya Upimaji naTathimini ya Elimu, Huduma ya Ukaguzi wa Elimu, Huduma za Maktaba na Huduma ya Urajisi wa Elimu.

## AFISI YA MRAJIS WA ELIMU

Afisi ya Mrajis wa Elimu, iko chini ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, ambayo inaongozwa na Mrajis wa Elimu ambaye pia ni Katibu wa Baraza la Elimu. Majukumu makubwa ya Baraza la Elimu ni haya yafuatayo:-

*(i)* Kumsaidia Waziri wa Elimu katika kutelekeza Sera ya Taifa ya Elimu;

*(ii)* Upangaji wa Huduma za Elimu hapa Zanzibar na masomo ambayo yatatolewa katika aina mbali mbali;

*(iii)* Sheria yoyote inayohusiana au kuathiri elimu;

*(iv)* Mambo mengine yoyote yanayohusiana na elimu;

*(v)* Usajili wa Skuli za Serikali na Binafsi;

*(vi)* Usajili wa Walimu;

*(vii)* Utoaji wa Leseni za Walimu;

*(viii)* Kusimamia shughuli za Bodi za Elimu za Mikoa na Wilaya;

*(ix)* Kushughulikia na kuweka kumbukumbu za Kesi za Wanafunzi waliopata ujauzito, walioolewa pamoja na kesi za Udhalilishaji za Wanafunzi.

## CHANGAMOTO ZA AFISI YA MRAJIS WA ELIMU

*(a)* Ufinyu wa Afisi kwa wafanyakazi wake hasa kwa upande wa Pemba.

*(b)* Uhaba wa vitendeakazi ikiwemo mashine ya kutengeneza Leseni za Elektroniki, komputa, gari, vespa.

*(c)* Baadhi ya walimu wa Skuli Binafsi hawapasishi leseni zao.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuiingizia fedha za OC Afisi ya Mrajis wa Elimu kwa wakati na kwa mujibu wa bajeti, ili iweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

*(b)* Aidha, Kamati inaiomba Afisi ya Mrajis wa Elimu kuongeza kasi ya kufanya ukaguzi wa mara kwa mara, yaani ukaguzi wa kumshtukiza kwa kushirikiana na Afisi ya Mkaguzi wa Elimu, ili kuwabaini walimu ambao hawapasishi leseni zao hasa walimu wa skuli binafsi.

*(c)* Vile vile, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipatia vitendeakazi ikiwemo mashine maalum ya kutengeneza Leseni za Elektroniki, komputa, gari, vespa Afisi ya Mrajis wa Elimu, ili iweze kufanya kazi zake za kila siku katika hali nzuri.

*(d)* Kamati inaiomba Serikali kuitafutia jengo au sehemu nyengine kwa ajili ya Afisi ya Mrajis wa Elimu yenye mazingira rafiki ya kuweza kufanya kazi na kuondokana na hali ya ufinyu wa nafasi na kupelekea kushuka kwa ufanisi wa utendaji wa kazi.

## BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR

Baraza la Mitihani la Zanzibar limeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Namba 6 ya 2012 ambapo jukumu la Msingi la Baraza hilo ni kufanya Upimaji kwa wanafunzi, ili kujua kiwango cha maarifa, umahiri na mwelekeo waliopata baada ya kujifunza. Upimaji huu hufanyika kwa kuandaa na kusimamia Mitihani ya Taifa ya SMZ kwa kumaliza elimu kwa ngazi tofauti kama hivi ifuatavyo:-

*(i)* Elimu ya Msingi.

*(ii)* Elimu ya Sekondari ya Awali (Kidato cha Pili).

*(iii)* Mitihani ya Mafunzo ya Ualimu Ngazi ya Cheti na Stashahada.

*(iv)* Vile vile, kufanya tathmini ya matokeo ya Mitihani hiyo.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA MITIHANI LA ZANZIBAR**

*(a)* Kukosekana kwa kiwanda cha Baraza la Mitihani kwa ajili ya uchapaji wa mitihani, hivyo Baraza hulazimika kuchapisha mitihani katika viwanda vyengine, jambo ambalo linaweza kupunguza usiri wa mitihani, kuvuja kwa mitihani pamoja na kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kazi hizo.

*(b)* Baraza kutomiliki majengo kwa ajili ya Vituo vya Usahihishaji wa Mitihani, hali hii huleta usumbufu mkubwa katika zoezi la usahihishaji wa mitihani.

*(c)* Uhaba wa nafasi katika jengo la ofisi za Baraza kutokana kwa kuongezeka idadi ya wafanyakazi.

*(d)* Upungufu wa wataalamu wenye fani maalum kwa mfano, watakwimu, wachambuzi wa taarifa za mitihani pamoja na wataalamu wa masomo ya ufundi.

*(e)* Ongezeko la mimba na ndoa za utotoni katika skuli kwa Unguja na Pemba.

*(f)* Uwepo wa madeni ya wasahihishaji pamoja na wasimamizi wa mitihani.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto kuandaa kanzidata "database" ya uwekaji wa kumbukumbu sahihi na ufuatiliaji wa Kesi za Udhalilishaji kwa wanafunzi.

*(b)* Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuiomba Serikali kupatiwa maeneo kwa ajili ya kujenga majengo ya kusahihishia mitihani, ili

kuisaidia Serikali kuondokana na gharama kubwa na zisizo za lazima kwa kukodi majengo ya watu binafsi kwa ajili ya kusahihisha mitihani.

*(c)* Kamati pia inaendelea kuishauri Serikali kuajiri wataalamu wabobezi fani maalum kwa mfano, watakwimu, wachambuzi wa taarifa za mitihani pamoja na wataalamu wa masomo ya ufundi, kukosekana kwa wataalamu hao hupelekea Wizara ya Elimu kukodi wataalamu hao kutoka sekta binafsi.

## OFISI YA MKAGUZI WA ELIMU ZANZIBAR

Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu ni Wakala wa Serikali ulioanzishwa chini ya Sheria Namba 1 ya Mwaka 2018. Ofisi hii ina jukumu kubwa la kusimamia ubora wa Elimu kwa kufanya ukaguzi wa Elimu kwa Skuli zote za Maandalizi, Msingi na Sekondari zilizosajiliwa pamoja na Kufanya Ukaguzi katika Taasisi zinazotoa Mafunzo ya Ualimu, Vituo vya Elimu Mbadala na Elimu ya Watu Wazima na Taasisi za Elimu zilizosajiliwa zilizo nje ya Mfumo Rasmi wa Elimu.

## CHANGAMOTO ZA OFISI YA MKAGUZI WA ELIMU ZANZIBAR

*(a)* Ukosefu wa Majengo ya Ofisi. Sheria ya kuanzishwa kwa Ofisi imeanzisha ndani yake Ofisi za Ukaguzi za Mikoa. Ofisi hizi kwa sasa zipo kinadharia tu. Wakaguzi wamegawiwa kimikoa na wanatekeleza majukumu yao kwa mgawanyiko wa Mikoa. Hata hivyo, kiutendaji Mkoa wa Mjini Magharibi na Mkoa wa Kusini Unguja wapo katika jengo la Ofisi Kuu ambalo halina nafasi. Kwa upande wa Mkoa wa Kaskazini Unguja wapo katika chumba kimoja katika majengo ya Ofisi za SUZA – Beit – El – Ras ndicho ambacho kinatumika. Aidha, kwa upande wa Pemba hali ipo kama ilivyo Unguja wapo

katika jengo la Maktaba Chake Chake na kwa Wete wapo jengo la Ofisi ya Elimu Mkoa.

*(b)* Ukosefu wa usafiri wa kudumu kwa watendaji wa Ofisi pamoja na changamoto wakaguzi wa elimu hali inayopelekea wakati mwengine kushindwa kufika katika maeneo yao ya kazi kwa wakati.

*(c)* Ukosefu wa Stahiki za Wakuu wa Ukaguzi wa Mikoa na Wakaguzi wa Elimu, suala hili bado ni changamoto hali inayopelekea kuwavunja moyo watendaji wetu wa ndani pamoja na wakaguzi wetu wa elimu. Wakaguzi ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu sana na mwisho kuwapelekea pia hata kukosa morali ya kufanya kazi.

*(d)* Upungufu wa watendaji idadi iliopo sasa ya wakaguzi wa elimu 88 (Pemba 28 na Unguja 60) ukizingatia uhitaji uliopo kwa idadi hii bado haijakidhi mahitaji ya Ofisi na ipo haja idadi hii kuongezeka. Kwani kwa sasa mkaguzi 1 anaweza kukagua skuli zaidi ya 1 kutokana na uhaba ulipo na hatimae mwisho kukosa hata muda wa kuwasilisha ripoti ya ukaguzi kwa muda na pia kwa upande mwengine mkaguzi huyo huyo ni mwalimu wa Skuli changamoto hii pia inawaathiri Watoto kukosa masomo.

*(e)* Mahudhurio ya walimu sio mazuri kutokana na walimu wengi hupangiwa skuli za mbali na maeneo wanayoishi.

*(f)* Madeni makubwa wanayodai wakaguzi wetu wa elimu kwa muda mrefu sana na miaka mingi kupita wakaguzi wa elimu hawajalipwa stahiki zao pamoja na posho za kufanya kazi kwenda katika Skuli za vijijini na visiwani hali inayowapelekea kufanya kazi katika mazingira magumu na wakati mwengine mtu kushindwa kufika katika skuli alizopangiwa kuzifanyia ukaguzi huo.

*(g)* Ukosefu wa mafunzo kwa wakaguzi wetu na kubakia kufanya kazi kimazoea bila ya ujuzi wala taaluma yoyote ya ukaguzi.

*(h)* Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri baina ya walimu wanaokaguliwa na wakaguzi wa elimu pale anapofika Skuli kwa ajili ya kufanya ukaguzi.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuliangalia upya suala la bajeti ndogo ya uendeshaji inayotengewa Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu Zanzibar hali inayopelekea kushindwa kufanya kazi zake ipasavyo kama Sheria inavyoelekeza.

*(b)* Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kulitafutia ufumbuzi wa haraka changamoto ya madeni ya wakaguzi wetu wa ndani yanayotokana na kazi ya ukaguzi unaofanya katika Skuli zetu za Maandalizi, Msingi na Sekondari.

*(c)* Kamati pia inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kuwapatia maeneo Ofisi ya Mkaguzi wa Elimu Zanzibar kwa ajili kujenga majengo ya Ofisi hiyo, ili waondokana na kadhi ya kujibanabana katika Ofisi za Taasisi nyengine kama ilivyo sasa ambapo katika Mikoa yote iliopo Unguja na Pemba hawana Ofisi za uhakika na kudumu.

*(d)* Kamati tena inaiomba Serikali kuliangalia kwa ukaribu suala zima la kusimamishwa kwa ajira Serikalini, kwani Kamati imebaini chanzo cha matokeo mabaya ya Ufaulu Zanzibar katika Skuli zetu yanatokana pia kukosekana kwa kufanyika kwa ukaguzi kwa wakati. Kwa sababu pale ukaguzi unapofanyika Wizara inapata kujua wapi kuna changamoto ya walimu na kwa kiasi gani inahitaji ufumbuzi wa haraka.

## KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA

Kitengo cha Elimu Mjumuisho kinafanya kazi katika maeneo mawili makubwa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha ambazo zinawafundisha manafunzi nyenzo mbali mbali, ili kuweza kukabiliana na changamoto katika Maisha. Kamati katika kufanya kazi zake ilipata fursa ya kutembelea Skuli ya Mwanakwerekwe "H" na Mwanakwerekwe "F" pamoja na Skuli ya Kisiwandui kwa upande wa Unguja. Skuli ambazo zinatoa Elimu Mjumuisho kwa Watoto wenye Ulemavu, ili kuweza kujionea hali halisi ya mafanikio yanayopatikana pamoja na changamoto.

## CHANGAMOTO ZA KITENGO CHA ELIMU MJUMUISHO NA STADI ZA MAISHA

*(a)* Kitengo kinakabiliwa na uhaba wa watendaji pamoja na vifaa ikiwemo usafiri, kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi.

*(b)* Ofisi ya kufanyia kazi zao sio rafiki kwa watu wenye ulemavu.

*(c)* Uchache wa fedha za OC kwa lengo la kuweza kutekeleza majukumu ya Kitengo kwa ufanisi kwa Unguja na Pemba.

*(d)* Idadi kubwa ya wanafunzi katika madarasa hali inayopelekea walimu kushindwa kuwahudumia wanafunzi hao katika uangalizi unaohitajika kwa wakati.

*(e)* Ongezeko la vitendo vya Udhalilishaji kwa wanafunzi bado ni tatizo kubwa kutokana na baadhi ya walimu na jamii kwa ujumla kuendelea kuwadhalilisha wanafunzi hao.

*(f)* Kukosekana kwa uelewa wa lugha za alama, wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia hawafahamu lugha ya alama kutokana na wanafunzi hao kutopata

maneno yote wakati wa kuandika hivyo hupelekea idadi ya ufaulu wa masomo inakuwa ni ndogo.

*(g)* Ukosefu wa miundombinu Rafiki ya kufundishia wanafunzi ambapo madarasa yanayotumika kwa wanafunzi hawa ni chakavu, ukosefu wa vikalio pamoja na vifaa vya kujifunzia.

*(h)* Kukosekana kwa mitaala ya kufundia wanafunzi wenye ulemavu wa kusikia pamoja na wale wenye matatizo ya akili.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inakipongeza Kitengo cha Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha kwa kufanya kazi licha ya kukabiliwa na changamoto mbali mbali, kwa ajili ya kuhakikisha kwamba wanatoa huduma tofauti kwa jamii.

*(b)* Aidha, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwamba Walimu wa Elimu Mjumuisho na Stadi za Maisha ni vyema wakapunguziwa vipindi kwa masomo ya kawaida na badala yake wakapata muda wa kutosha kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi masomo ya Elimu Mjumuisho pamoja na Stadi za Maisha.

*(c)* Kamati, inasikitishwa na muamko mdogo wa jamii wakiwemo baadhi ya walimu pamoja na wazazi kutokuwa na ujasiri wa kueleza au kufichua vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto kutokana na sababu ikiwemo muhali, kumalizwa kwa masuala hayo chini kwa chini, kwani mara nyingi masuala hayo hufanywa na watu wa karibu kama vile wazazi wenyewe au jamaa wa karibu ama majirani na kadhalika. Kwa kweli, hali hiyo inapelekea kuendelea kwa vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na watoto. Hivyo ni vyema kuachana na masuala ya muhali, kumaliza masuala hayo kinyume na

utaratibu, wahusika kutoa taaluma kwa wananchi na jamii kwa ujumla kuhusu kupinga vitendo vya udhalilisha kwa wanawake na watoto.

*(d)* Vile vile, Kamati inapendekeza kuhusu Masomo ya Vyuo vya Kur-aan, kwa lengo la wanafunzi kuweza kupata elimu ya Dini kwa ufanisi zaidi, ikiwemo Walimu kupatiwa mafunzo ya kutosha, vifaa, miongozo na mitaala pamoja na kuwepo kwa mashirikiano miongoni mwa taasisi za Serikali zinazoshughulikia masuala ya elimu ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Afisi ya Mufti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pamoja na Taasisi nyengine za Dini ya Kiislamu za ndani na nje ya nchi.

*(e)* Kamati, inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuharakisha ukamilishaji wa Miradi ya Ujenzi wa Skuli za Mjumuisho kwani watoto hawa nao wanahitaji mazingira bora ya kujifunzia, ili nao wajisikie na kuona jitihada za Serikali yao inavyowathamini na kuwapenda.

## C. PROGRAMU YA UONGOZI NA UTAWALA

Programu hii inahusika na Idara ya Utumishi na Uendeshaji, Idara ya Mipango, Sera na Tafiti za Wizara na Ofisi ya Elimu Pemba. Ambapo Kamati ilipokuwa ikitekeleza majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni imebaini yafuatayo:-

*(i)* Uhaba wa rasilimali watu katika Skuli pamoja na Taasisi zilizo chini ya usimamizi wa Wizara hii;

*(ii)* Kuchelewa kwa kukamilika kwa wakati baadhi ya Miradi mingi ya Ujenzi inayotekelezwa katika Wizara hii. Mfano, Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Amali Makunduchi, ambapo hadi tunawasilisha ripoti hii

mradi huu haujakamilika wa kukabidhiwa kutokana na kasoro mbali mbali, hali inayopelekea hasara kubwa kwa Serikali;

*(iii)* Kukosekana kwa Mitaala ya Watu Wenye Ulemavu wa Akili na Uoni;

*(iv)* Uwepo wa maslahi madogo kwa walimu pamoja na watendaji wa Wizara hii;

*(v)* Kutokuwepo kwa miundombinu Rafiki na yenye kufika katika baadhi ya majengo yetu ya Skuli za Maandalizi, Msingi hadi Sekondari hali inayowasababishia Watu Wenye Ulemavu kusoma katika mazingira magumu;

*(vi)* Kutokuwepo kwa usimamizi ulioimara katika utekelezaji wa Miradi ya Ujenzi wa Skuli kwa Unguja na Pemba. Hii inatokana na kukosekana kwa mafunzo kwa wakandarasi wetu wa Wizara hali inayopelekea kushindwa kusimamia miradi hiyo ipasavyo;

*(vii)* Kuchelewa kufanya ukarabati kwa baadhi ya Skuli zetu za Unguja na Pemba, ambapo ukiangali hali majengo yetu yote si ya kuridhisha kukaa watoto na kusomea. Mfano Skuli ya Ufundi Kengeja;

*(viii)* Kutokuwepo kwa madarasa maalum kwa ajili ya mafunzo ya amali kwa Watu Wenye Ulemavu;

*(ix)* Uhaba wa vikalio pamoja na vitabu vya kusomea katika baadhi ya Skuli yetu. Mfano halisi ni Skuli ya Mwanakwerekwe "H" na Mwanakwerekwe "F".

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

*(a)* Kamati, inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kutekeleza majukumu yake ya kila siku kwa kuzingatia Sheria, Kanuni pamoja na Taratibu

kwa lengo la kuweza kuleta ufanisi mkubwa zaidi kwa maslahi mapama ya jamii pamoja na Serikali kwa jumla.

*(b)* Vile vile, Kamati inapendekeza kwa Serikali kutafutwa Wakandarasi wenye uwezo, wazalendo pamoja na uaminifu katika kushughulikia Miradi ya Maendeleo kwa lengo la kuweza kukamilisha miradi hiyo kwa wakati tena yenye kiwango. Aidha, Kamati inasisitiza kwa Uongozi wa ZBA kufanya kazi ya kuwasimamia wakandarasi na kuwa makini wakati wanapotekeleza majukumu yao, ili lengo lililokusudiwa lipatikane kwa wakati na kiwango bora.

*(c)* Kamati, inaushauri Uongozi wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kushirikiana na Chuo Kikuu cha Taifa (*SUZA*) pamoja na jamii kwa ujumla katika kuwahamasisha wanafunzi kusoma masomo ya Sayansi kwa lengo la kupata wataalamu wengi zaidi wa Sayansi kwa lengo la kuwa na wataalamu wengi zaidi wazawa, yaani Wazanzibari kwa ajili ya kupunguza tatizo la wataalamu wa Sayansi katika taasisi tofauti za Serikali ndani ya nchi yetu na kupata maendeleo ya haraka kwa kuwatumia wataalamu wetu.

*(d)* Kamati, inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika suala la kuandaa na kuchapisha vitabu pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia kuwazingatia watu wenye ulemavu wakiwemo watu wenye ulemavu wa macho, kwa kuwapatia vifaa ikiwemo vitabu vya nukta nundu, mashine za kuchapia pamoja na vyengine, ili kuweza kupata elimu ambayo ni haki yao kama binaadamu au raia wengine wa Zanzibar.

*(e)* Aidha, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuweka mkazo katika kuboresha miundombinu ya majengo kwa ngazi ya Elimu ya Msingi, kwani hali halisi ya msongamano wa wanafunzi haiko vizuri, yaani darasa moja wanafunzi 60 na zaidi. Kwa kweli, hali ambao haiwezi kuleta ufanisi kwa kiasi kikubwa na matokeo yake wanafunzi wengi

wanamaliza elimu ya msingi wakiwa hawajapata lile lengo lililokusudiwa kwa ngazi hiyo ya elimu, yaani zile "K-3", (Kuhesabu, Kusoma na Kuandika).

*(f)* Kamati, inasisitiza kuwepo kwa mashirikiano mazuri baina ya Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo katika suala zima la michezo kwa wanafunzi au vijana wetu kuanza katika ngazi ya Skuli za Msingi pamoja na kurejeshwa kwa mashindano mbali mbali yaliyokuwepo hapo zamani. Kwa mfano, Mashindano ya Wilaya, Mikoa pamoja na Taifa kwa ujumla, kwa lengo la kuibua vipaji vipya tofauti kwa michezo tofauti kwa vijana wetu na kupata vijana au wanamichezo wengi wenye vipaji mapema, yaani tokea ngazi ya Skuli za Msingi.

*(g)* Pia, Kamati inatoa wito kwa jamii kuwa na mashirikiano mazuri na ya karibu na walimu katika suala zima la kudhibiti utoro kwa wanafunzi wetu pamoja na kuwa na nidhamu. Kwa kweli, baadhi ya wanafunzi hawana nidhamu ikiwemo kutoroka skuli, kwa maana ya kutohudhuria au kuhudhuria baadhi ya siku ama nusu siku, kuacha kuandika masomo wanayosomeshwa madarasani, kuvaa nguo ambazo haziruhusiwi pamoja na mambo mengine. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaona ni vyema na busara kwa jamii kuwa karibu na walimu kwa lengo la kuweza kushirikiana kwa pamoja katika kuwajenga wanafunzi ama vijana wetu katika maadili mema na kushughulikia masomo na kupata wataalamu wa sasa na baadaye kwa Taifa letu.

*(h)* Kamati, inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kujenga uzio pamoja na kufanya usafi eneo la mazingira yanayoizunguka Skuli ya Sekondari ya Hasnu Makame kwa kushirikiana na Uongozi wa Wilaya kwa kuwatumia wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo, kwa lengo la kuiweka au kuifanya skuli hiyo iwe katika mazingira rafiki ya kuweza kufundishia na kujifunzia, kuwepo kwa walinzi pamoja na utaratibu wa kuingia na kutoka kwa wanafunzi.

*(i)* Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuwa na mtaalamu kwa ajili ya kuyaangalia majengo ya skuli kwa ngazi ya Wilaya kwa lengo la kuyahifadhi, kuyatunza pindi inapotokea hitilafu na kuweza kutumika kwa muda mrefu zaidi.

*(j)* Kamati, inaiomba Serikali kuhusu walimu au wakufunzi ama wataalamu wa *SUZA* kuongezewa muda wa kustaafu kama ilivyo kwenye vyuo vikuu vyengine duniani, yaani wataalamu kama hao hutumikia mpaka miaka 70 badala ya 60 ambao ndio umri wa kustaafu kwa utumishi kutokana na utaalamu wao.

*(k)* Vile vile, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kupitia Uongozi wa Skuli ya Ufundi Kengeja kwamba kuhusu uchakavu wa majengo pamoja na samani za Skuli hiyo ni vyema wanafunzi kwa kushirikiana na walimu kuweza kufanya marekebisho ikiwa ni sehemu ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi hao, ili kuweza kupata kufanya marekebisho ya majengo pamoja na samani kwa ufanisi zaidi.

*(l)* Kamati, inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuifanyia matengenezo Skuli ya Ufundi Kengeja kutokana na uchakavu wa majengo, samani, kuongeza idadi ya madarasa, workshop, dakhalia, kujenga uzio wa matofali, kuipatia usafiri wa gari skuli hiyo.

*(m)* Kamati, inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuzipatia ufumbuzi changamoto ikiwemo suala la uchache wa vitabu, uhaba wa walimu pamoja na kutengeneza miundombinu rafiki kwa ajili ya watu wenye ulemavu kuweza kufaidika na huduma za Shirika la Maktaba Pemba.

*(n)* Vile vile, Kamati inaishauri Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuhusu Masomo ya Vyuo vya Kur-aan, kwa lengo la wanafunzi kuweza kupata elimu ya Dini kwa ufanisi zaidi, ikiwemo Walimu kupatiwa mafunzo ya kutosha, vifaa, miongozo na mitaala pamoja na kuwepo kwa mashirikiano miongoni

mwa taasisi za Serikali zinazoshughulikia masuala ya elimu ikiwemo Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Afisi ya Mufti, Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana pamoja na Taasisi nyengine za Dini ya Kiislamu za ndani na nje ya nchi.

*(o)* Aidha, Kamati inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuifanyia matengenezo Skuli ya Msingi ya Kisiwandui, ili iweze kukabiliana na changamoto ya uchache wa madarasa na idadi kubwa ya wanafunzi, ili kuepukana na tatizo hilo la ufinyu wa madarasa katika Skuli hiyo na ufanisi zaidi uweze kupatikana.

*(p)* Kamati, inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kuipatia walimu pamoja na vifaa vya kujifunzia na kufundishia Skuli ya Msingi ya Kisiwandui, kwa lengo la kuweza kuwapatia elimu wanafunzi kwa ufanisi mkubwa zaidi wakiwe na wale wanafunzi wenye ulemavu wa Uoni pamoja na Akili.

*(q)* Kamati, inaiomba Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali kwa kuwaekea Darasa Maalum la Kazi za Amali kwa wanafunzi wenye ulemavu, ambapo baada ya kumaliza masomo ya Elimu ya Lazima basi ni vyema kuendelea kwenye darasa hilo, ili kuweza kupata kujifunza Kazi za Amali na Stadi za Maisha ikiwemo kazi na mikono, kama vile ufumaji, ushoni, ufinyanzi na kadhalika.

*(r)* Kamati, inapendekeza Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali katika kuandaa Mitaala Mipya kuzingatia uanzishaji wa Masomo ya Mafunzo ya "Self Defence" pamoja na Uraia kwa wanafunzi wetu ni jambo muhimu, kwa ajili ya wanafunzi wetu kuweza kukabiliana na mazingira. Kwa mfano, mafunzo ya Kuogelea, Karati, Namna ya kujikinga na Ukatili na Udhalilishaji wa wanawake na watoto.

## 4. WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo inaundwa na Sekta Nne ambazo ni:

*(i)* Sekta ya Habari;
*(ii)* Sekta ya Vijana;
*(iii)* Sekta ya Utamaduni; na
*(iv)* Sekta ya Michezo.

Ndani sekta hizo kuna Idara, Mabaraza, Mashirika, Tume, Kampuni, Wakala na Afisi Kuu Pemba kama ifuatavyo:-

**SEKTA YA HABARI**

*(a)* Idara ya Habari na Maelezo;
*(b)* Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*);
*(c)* Tume ya Utangazaji Zanzibar;
*(d)* Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar (*ZGPA*);
*(e)* Kampuni ya Kuunganisha na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (*ZMUX*);
*(f)* Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar.

**SEKTA YA VIJANA**

*(i)* Idara ya Maendeleo ya Vijana.
*(ii)* Baraza la Vijana Zanzibar.

**SEKTA YA UTAMADUNI**

*(i)* Idara ya Utamaduni;
*(ii)* Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni;
*(iii)* Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar (*COSOZA*);
*(iv)* Baraza la Kiswahili (BAKIZA).

**SEKTA YA MICHEZO**

*(i)* Idara ya Michezo.
*(ii)* Baraza la Taifa la Michezo Zanzibar (BTMZ).
*(iii)* Idara ya Mipango, Sera na Utafiti.
*(iv)* Idara ya Utumishi na Uendeshaji.
*(v)* Afisi Kuu Pemba.

## A. PROGRAMU YA MAENDELEO YA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

Programu hii inaundwa na Programu Ndogo Mbili ambazo ni Upatikanaji na Usambazaji wa Habari na Utangazi na Uchapaji.

### I. PROGRAMU NDOGO YA UPATIKANAJI NA USAMBAZAJI WA HABARI

Programu Ndogo hii inatekelezwa kupitia Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), Idara ya Habari Maelezo, Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) pamoja na Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui (ZMUX). Kamati ilifanya kazi kwa karibu na Taasisi hizi pamoja na Mashirika na kuona changamoto mbali mbali katika utekelezaji wa majukumu yao.

**SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (*ZBC*)**

Shirika la Utangazaji Zanzibar (*Zanzibar Broadcusting Coperation - ZBC)* ni muungano wa zilizokuwa taasisi *mbili (2)* kubwa za habari nchini ambazo ni: Sauti ya Tanzania Zanzibar *(STZ)* na Idara ya Televisheni *(TVZ)*. Taasisi hizi ziliunganishwa kupitia Sheria ya Shirika la Utangazaji Zanzibar, Nambari 4 ya Mwaka 2013.

**MAJUKUMU YA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (ZBC)**

*(i)* Kutoa habari;
*(ii)* Kuelimisha;
*(iii)* Kuburudisha;
*(iv)* Kushajihisha au kuhamasisha jamii;

*(v)* Kukosoa jamii.

## CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA UTANGAZAJI ZANZIBAR (*ZBC*)

*(a)* Uhaba wa Rasilimali watu na vifaa kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi katika vituo vyote vya ZBC ikiwemo Unguja, Pemba na Dar-es-Salaam.

*(b)* Bajeti ndogo ya kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu ya *ZBC* – TV na Redio ikiwemo kuandaa vipindi vya nje ya studio. Hali inayowapelekea watendaji wa ZBC kushindwa kufanya vipindi vipya kutokana na uhaba wa bajeti, ambapo vipindi hurudiwa kwa muda mrefu.

*(c)* Kuchelewa kupata Taarifa za kazi za Serikali na *ZBC* ni chombo na mdomo wa Serikali na badala yake vyombo binafsi kupata taarifa mapema na kufika mwanzo kwenye kazi.

*(d)* Vifaa vilivyofungwa Ofisi ya ZBC Pemba vimepitwa na wakati.

*(e)* Kutokuwepo kwa Muundo wa Utumishi katika Shirika la ZBC.

*(f)* Ufinyu wa ofisi katika Kituo cha Dar-es-Salaam.

*(g)* Kukosekana kwa Ofisi ya ZBC Makamu Makuu ya Nchi Dodoma.

*(h)* Maslahi madogo ya wafanyakazi hali inayowapelekea kufanya kazi katika mazingira magumu, ambapo wakihitajika kwenda kufanya kazi nje ya ofisi malipo ni shilingi 5,000/-.

*(i)* Kuwepo kwa mashirikiano madogo baina ya watendaji wa ZBC na Idara ya Mawasiliano Ikulu.

*(j)* Uhaba wa wataalamu wenye fani maalum katika Tasnia ya Habari.

*(k)* Kutokuwepo kwa posho la mazingira magumu kwa madereva wa Shirika la Utangazaji.

*(l)* Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa Ujenzi wa Jengo la ZBC Pemba. Kamati hadi inasoma ripoti hii Mradi huu haujakabidhiwa kwa Wizara na muda wa utekelezaji kwa mujibu wa mkataba ushamaliza.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inaupongeza Uongozi pamoja na watendaji wa Shirika la Utangazaji (*ZBC*) kwa kufanya kazi zao licha ya kukabiliwa changamoto mbali mbali za kiutendaji, lakini wafanyakazi hao wanafanya kazi zao kwa moyo wa uzalendo katika kutangaza Sera na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

*(b)* Kamati, inaiomba Idara ya Mawasiliano Ikulu kufanya kazi kwa karibu na Uongozi wa Shirika la Utangazaji (*ZBC*), kwani wao ndio chombo na mdomo wa kuyatangaza masuala ya yanayotekelezwa na Serikali. Ambapo Kamati imebaini kuna shughuli nyingi za Viongozi wa Kitaifa zinafanyika ndani na nje ya nchi na Shirika kuchelewa kupata taarifa mapema, hali inayowapelekea kuchelewa kufika katika maeneo ya matukio kwa wakati muafaka.

*(c)* Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuongeza Bajeti kwa Shirika la Utangazaji (*ZBC*) kwa lengo la kuweza kutekeleza majukumu yao ya kila siku.

*(d)* Kamati inaziomba Taasisi zote za Serikali zinazodaiwa na Shirika la *ZBC* kufanya malipo kwa haraka, ili Shirika liweze kujiendesha kibiashara na sio huduma kama ilivyozoeleka.

*(e)* Pia, Kamati inausisitiza Uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutatua tatizo la rasilimali watu, vifaa pamoja na mafunzo kazini kwa watendaji wa Shirika la Utangazaji (*ZBC*), ili kuweza kuendana na soko la ushindani la kibiashara duniani katika Tasnia ya Habari.

(f) Kamati inaiomba Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikanili kuipatia nafasi za ajira Shirika la Utangazaji Zanzibar, ili kuweza kuajiri wataalamu wabobezi katika fani ya utangazaji wa habari, ili Shirika liweze kwenda sambamba na mabadiliko ya teknolojia ya habari.

(g) Kamati, inaushauri Uongozi wa Shirika la Utangazaji (*ZBC*) kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa Muundo wa Utumishi wa Shirika kwa haraka iwezekanavyo na kuuwasilisha Tume ya Utumishi Serikalini kwa ajili ya kupatiwa Baraka, kama inavyofahamika kukosekana kwa Muundo wa Utumishi katika Taasisi yoyote ya Serikali kunapelekea kuwakosesha haki pamoja na stahiki zao watendaji wa chini.

(h) Kamati inaiomba Wizara kukaa na Chuo cha Mafunzo kuharakisha ukamilishaji wa utekelezaji wa Ujenzi wa Mradi wa Jengo la Studio za ZBC Pemba kwani Mradi huu imeshachukua muda mrefu bila ya kukamilika.

**SHIRIKA LA MAGAZETI YA SERIKALI ZANZIBAR**

Shirika la Magazeti ya Serikali Zanzibar limeanzishwa kwa Sheria Nambari 11 ya mwaka 2008. Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) limefanikiwa kuchapisha Gazeti la kila siku la Zanzibar Leo, Magazeti ya kila wiki Zanzibar Mail, na Zaspoti, Gazeti la kila mwezi Zanzibar Leo Wanawake na Zanzibar Leo Jumapili na kuyasambaza katika mikoa yote ya Zanzibar pamoja na baadhi ya mikoa ya Tanzania Bara kwa lengo la kutoa habari, kuelimisha jamii kuhusu masuala ya kiuchumi, kijamii na kisiasa halikadhalika kutangaza Sera za Serikali pamoja na burudani na michezo.

**CHANGAMOTO ZA SHIRIKA LA MAGAZETI ZANZIBAR**

*(i)* Kuongezeka kwa gharama kubwa za uchapaji Dar-es-Salaam na pia kuna hatari ya kuongezeka kwa gharama hizo zaidi kutokana na kupanda kwa gharama za malighafi.

*(ii)* Mauzo madogo ya magazeti ambapo fedha za matangazo ndizo zinafidia gharama za uchapishaji ambazo nazo pia hazikidhi mahitaji ya Shirika katika uendeshaji shughuli zake za kila siku.

*(iii)* Ukosefu wa matangazo katika magazeti ya Zanzibar Mail, Zanzibar Leo Wanawake na Zaspoti, hivyo matangazo yanayopatikana kupitia Zanzibar Leo ndio wanayosaidia uchapishaji wa magazeti hayo.

*(iv)* Shirika la Magazeti ya Serikali limeanzishwa bila ya kupewa mtaji wa kujiendeleza. Ambapo Shirika hutumia fedha zao za makusanyo ya ndani, hata hivyo hazikidhi na kupelekea kufanya kazi katika mazingira magumu.

*(v)* Shirika kiuhalisia linatakiwa lipatiwe Shilingi Bilioni 2 kwa kila mwaka kwa ajili ya uchapishaji na usambazaji wa magazeti yake ya kila siku, wiki na kila mwezi kufikia nchi nzima Zanzibar na Tanzania Bara.

*(vi)* Uwepo wa madeni wa kubwa na ya muda mrefu ya uchapaji wa kazi mbali mbali za Taasisi za Serikali na Mashirika ya Umma na watu Binafsi hali inayowasababishia kupata makusanyo madogo. Madeni haya yanajumuisha wanayodai na wanayodaiwa Shirika kama Shirika:

- ✓ Ambapo kwa ujumla Shirika linadai jumla ya **Shilingi 2,445,808,557/=** kwa Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Taasisi ya Serikali ya Jamhuri wa Muungano wa Tanzania. Deni hili linajumuisha na madeni ya zamani.
- ✓ Pia, kwa Julai – Septemba, Shirika limetoa matangazo yenye thamani ya Tanzania Shilingi **181,084,437/=** ambapo fedha zilizolipwa ni **52,085,885/=.** Shirika linadai **128,998,552/=.**

- ✓ Vile vile, Shirika hadi kufikia mwezi wa Septemba, 2021 linadaiwa Shilingi **392,861,881/=** ambapo Wakala wa Uchapaji wanawadai Shirika Shilingi **34,153,750/=** fedha hizo ni deni la uchapaji wa Magazeti. Pia, Shirika la Magazeti linadaiwa **Shilingi 289,900,000/=** na Shirika la Uchapaji Tanzania (TSN) zikiwa ni deni la uchapaji wa gazeti la Zanzibar Leo na Zaspoti deni hili ni la tokea mwaka 2016.
- ✓ Sambamba na hilo, Mwezi wa Julai – Septemba, 2021 Shirika linadaiwa Shilingi **68,808,131/=** kwa ajili ya uchapaji, usambazaji na uendeshaji wa shughuli za Shirika.

*(vii)* Pia, Shirika linakabiliwa na changamoto ya Bajeti ndogo ambapo haikidhi mahitaji ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Shirika kwa mwaka husika.

*(viii)* Ukosefu wa soko la uhakika la ndani na nje ya Zanzibar.

*(ix)* Kuchelewa kubadilishwa kwa bei ya Uuzwaji wa Gazeti la Zanzibar, ambapo bei inayotumika kuuzia ni shilingi 500 tu. Ambapo bei hii imeanza kutumika tangu mwaka 2002 hadi sasa imeshapitwa na wakati.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati imeupongeza Uongozi wa Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) kwa muda mfupi kwa kuweza kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya changamoto zinazolikabili shirika hilo ikiwemo kuongeza idadi ya mikoa mipya ya Tanzania Bara usambazaji wa gazeti la Zanzibar Leo, kupata ofisi mpya Dodoma pamoja na gazeti la Zanzibar Leo kutumia mitandao ya kijamii kama vile '*WhatsApp*, *Twitter*, *Instagram* pamoja na *Facebook'*.

*(b)* Aidha, Kamati imetoa ushauri kufanya utafiti kuhusu maeneo mengine ndani ya Zanzibar na Tanzania Bara ambayo bado gazeti la Zanzibar Leo halifiki,

kwa lengo la kuweza kulifikisha, ili wananchi wa maeneo hayo waweze kupata habari pamoja na taarifa mbali mbali zinazoandikwa kwenye gazeti hilo.

*(c)* Vile vile, Kamati inasisitiza kuhusiana na maamuzi ya Serikali kwa taasisi zote za Serikali kutoa matangazo yao kupitia vyombo vya umma vya Serikali, kwa lengo la kuvitumia vyombo hivyo pamoja na kuweza kupata mapato, ili kuweza kujiendesha kwa ufanisi zaidi.

*(d)* Kamati, inapendekeza kuhusu taarifa za Viongozi Wakuu ziwasilishwa katika ofisi za Shirika la Magazeti ya Serikali (SMS) kwa ajili ya kufanyiwa kazi kwa uharaka na ufanisi zaidi kuliko hali ilivyo sasa.

*(e)* Pia, Kamati inaiomba Serikali kulipatia Shirika la Magazeti ya Serikali rasilimali watu pamoja na vifaa ikiwemo Posho Maalum, usafiri pamoja na fedha za OC, kwa ajili ya kuweza kutekeleza kazi zake kwa ufanisi zaidi.

## KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX)

Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX) ni Kampuni ya Serikali iliyoanzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Makampuni Nam. 15 ya Mwaka 2013, na baadae kufanyiwa mapitio Mwaka 2018. Kampuni hii ni miongoni mwa Taasisi sita (6) zinazounda Sekta ya Habari na inatekeleza majukumu yake chini ya Programu ya Maendeleo ya Habari, Utangazaji na Uchapaji. Majukumu makuu ya Kampuni hii ya Uuunganishaji na Usambazaji wa Maudhui Zanzibar (ZMUX) ni pamoja na kuanzisha na kuendeleza biashara ya maudhui katika mfumo wa dijitali, kuendeleza miundombinu ya upokeaji na usambazaji wa maudhui (content), kuendeleza na kuimarisha huduma za utangazaji za ndani na nje ya nchi.

## CHANGAMOTO ZA KAMPUNI YA UUNGANISHAJI NA USAMBAZAJI WA MAUDHUI ZANZIBAR (ZMUX)

*(i)* Uchakavu wa miundombinu ya uunganishaji na usambazaji maudhui.

*(ii)* Kampuni kutomiliki minara yake ya kurushia maudhui.

*(iii)* Kutokuwepo kwa udhibiti wa bei za watoa huduma hasa kati ya Taasisi za Serikali na ZMUX. ZMUX ilifanya mazungumzo na ZICTIA juu ya kupunguza gharama za huduma ya matumizi ya Mkongo ambapo kwa mwezi wanawatoza shilingi milioni 50,000,000/= hali inayopelekea Kampuni hii kufanya kazi katika mazingira magumu.

*(iv)* Kutokuwepo kwa mikataba ya Minara baina ya ZMUX na Kampuni Binafsi.

*(v)* Kampuni kufanya kazi zaidi katika kutoa huduma kwa wananchi na sio biashara kama ilivyokusudiwa, ambapo kupelekea hata kukosa masoko ya watazamaji wa ndani na nje ya Zanzibar.

*(vi)* ZMUX inafanya kazi kinyume na taratibu za Sheria, kwani hadi Kamati inapokea taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa kipindi cha Oktoba – Disemba, 2021 Kampuni hii haina Bodi wa Wakurugenzi.

*(vii)* Urushaji wa vipindi wa Taasisi za Serikali bure. Hii inapelekea ZMUX kuzorota kiutendaji kwa sababu hiki ndio chanzo chao kikuu cha mapato ya Kampuni.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kufanya utafiti wa kina na kitaalamu katika maeneo yote yatakayokusudiwa kujengwa minara kwa ajili ya kurushia matangazo.

*(b)* Kamati inaishari Serikali kuandaa kikao cha mazungumzo ya pamoja kwa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo na Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi juu ya suala zima la upandishaji wa bei kati ya Taasisi za Serikali kinyume na utaratibu. Kamati kutokana na kadhi hii haikufurahishwa kuona Taasisi za Serikali zinavutana katika utendaji, wakati wote wapo kwa ajili ya kutoa huduma na kuongeza pato la nchi.

*(c)* Pia, Kamati inaishauri Kampuni ya ZMUX kuandaa mpango madhubuti wa biashara "Business Plan" ili kuweza kuingia katika ushindani wa kutafuta masoko Duniani.

*(d)* Kamati inaiomba Serikali kuharakisha uteuzi wa Bodi ya Kampuni hii, kubakia kama ilivyo ni kuirudisha nyuma kiendeshaji na kimaamuzi, kwani kama inavyofahamika katika Taasisi kama hizi haziwezi kufanyakazi bila ya uwepo wa Bodi na Uongozi.

*(e)* Kamati, inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuwapatia mafunzo watendaji wa Kampuni ya Uunganishaji na Usambazaji Maudhui, ili waweze kuendana na mabadiliko ya teknolojia ya habari na mawasiliano.

## II. PROGRAMU NDOGO YA USIMAMIZI WA VYOMBO VYA HABARI, UTANGAZAJI NA UCHAPAJI

Programu hii inatekelezwa kupitia Taasisi Tatu Kuu ikiwemo Idara ya Habari Maelezo, Tume ya Utangazaji Zanzibar na Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.

### WAKALA WA SERIKALI WA UCHAPAJI ZANZIBAR

Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar ni moja ya Taasisi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliopo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Wakala umeanzishwa kwa mujibu wa Sheria Nam.12 ya Mwaka 2018. Majukumu Makuu ya Wakala ni kutoa huduma za uchapaji pamoja na uuzaji wa vifaa vya Ofisi na Kuandikia kwa Taasisi za Serikali na Binafsi.

**CHANGAMOTO ZA WAKALA WA UCHAPAJI ZANZIBAR**

*(a)* Uhaba wa rasilimali watu na vifaa kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar.

*(b)* Tatizo baadhi ya Taasisi za Serikali kutopeleka kazi zake kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar pamoja na kuchelewa kulipwa kwa wakati, hali hiyo kupelekea Wakala kushindwa kutekeleza kazi zao kwa ufanisi zaidi.

*(c)* Kutokuwa na ghala la kudumu Unguja na Pemba kwa ajili ya uendeshaji wa Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisi na Kuandikia.

*(d)* Taasisi nyingi za Serikali kutotumia huduma za Bohari ya Vifaa vya Ofisi na Kuandikia, ambapo Kamati imegundua ni baadhi tu taasisi ndio zinayotumia Bohari yetu ya Vifaa kwa ajili ya matumizi ya Ofisi ikiwemo:-

*(i)* Wakala wa Ulinzi (JKU);
*(ii)* Tume ya Uchaguzi Zanzibar;
*(iii)* Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali;
*(iv)* Bodi ya Mapato Zanzibar;
*(v)* Tume ya Utangazaji;
*(vi)* Mfuko wa Barabara Zanzibar;
*(vii)* Mamlaka ya Maji (ZAWA);
*(viii)* Tume ya Utumishi Serikalini;

*(ix)* Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango;

*(x)* Wakala wa Biashara na Mali Zanzibar;

*(xi)* Shirika la Meli Zanzibar;

*(xii)* Wakala wa Majengo Zanzibar;

*(xiii)* Wakala wa Miundombinu TEHAMA;

*(xiv)* Baraza la Manispaa Mjini;

*(xv)* Shirika la Biashara la Taifa Zanzibar (ZSTC);

*(xvi)* Baraza la Mji Kaskazini "B";

*(xvii)* Baraza la Mji Kati,

*(xviii)* Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar;

*(xix)* Baraza la Mji Kaskazini "A";

*(xx)* Mamlaka ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Umma;

*(xxi)* Shirika la Bima Zanzibar;

*(xxii)* Baraza la Manispaa Magharibi;

*(xxiii)* Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Mjini Magharibi;

*(xxiv)* Taasisi ya Viwango Zanzibar (ZBS);

*(xxv)* Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda; na

*(xxvi)* Baraza la Mitihani.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inaridhishwa na juhudi zinazoendelea kuchukuliwa na Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar kwa kuweza kununua baadhi ya mitambo pamoja na kuanza ujenzi wa jengo la ghorofa mbili (2) kwa ajili ya kuongeza nafasi kwa lengo la kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi ikiwemo maeneo ya kuweka au kufunga mitambo ya kisasa kama vile mitambo ya kuchapia madaftari na mengine.

*(b)* Vile vile, Kamati inaiomba Serikali kuipatia maghala Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar kwa upande wa Unguja na Pemba, kwa lengo la kuweza kutekeleza jukumu la kutoa Huduma za Bohari Kuu ya Vifaa vya Ofisi na Kuandikia kwa ufanisi zaidi na kuachana na kukodi.

*(c)* Pia, Kamati inauomba Uongozi wa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar kwa kushirikiana na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kulitafutia ufumbuzi suala la uhaba wa rasilimali watu na vifaa kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar, kwa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yake kwa vizuri zaidi na kwa ufanisi.

*(d)* Kamati, inaiomba Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Serikali zinapeleka kazi zake kwa Wakala wa Serikali wa Uchapaji Zanzibar kama Agizo la Serikali linavyoelekeza pamoja na kulipa kwa wakati kwa ajili ya Wakala kuweza kujitegemea na kujiendesha wenyewe na kuweza kufikia malengo iliyojipangia. Kwani Kamati imebaini sababu kubwa inayoikumba Wakala katika utekelezaji wa shughuli zake ni mrundikano wa madeni makubwa na yasiolipwa kwa muda mrefu, ambapo hadi Kamati tunaiwasilisha kwenu ripoti Wakala wadai Taasisi za Serikali na Binafsi kama inavyoonekana.

*(e)* Kamati inaupongeza Wakala wa Uchapaji kwa kazi kubwa ya uzalendo kwa Serikali ya kuongeza Mapato ya ndani ya nchi.

## B. PROGRAMU YA MAENDELEO YA VIJANA

Programu hii inaundwa na Idara ya Maendeleo ya Vijana pamoja na Baraza la Vijana. Ambapo Kamati hii katika kufanya kazi zake za ufuatiliajia wa utekelezaji wa Serikali kupitia Taasisi zake kwa mujibu wa Kanuni za Baraza la Wawakilishi (Toleo la 2020) imebaini mambo mbali mbali katika Baraza na Miradi inayotekeleza kupitia Vijana.

## BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR

Baraza la Vijana Zanzibar limeanzishwa chini ya Sheria Nambari 16 ya 2013 ya Baraza la Vijana Zanzibar na linasimamiwa na Katibu Mtendaji ambaye huteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Aidha, Baraza hili linaunda na Mkutano Mkuu wa Baraza Taifa, Mkutano Mkuu Wilaya Pamoja na Mkutano Mkuu Shehia.

## MAJUKUMU YA BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR

*(a)* Kuishauri Wizara katika masuala yote ynayohusiana na mipango ya maendeleo ya Vijana.

*(b)* Kushajihisha upatikanaji wa haki za Vijana pamoja na kupanua wigo endelevu wa maendeleo katika matumizi ya Sera, Sheria na Kanuni.

*(c)* Kuwezesha na kuimarisha mashirikiano miongoni mwa Jumuiya zilizosajiliwa za Vijana Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

*(d)* Kusaidia na kushajihisha vikundi vyenye maslahi na maendeleo ya Vijana katika kuanzisha mafunzo na mipango ya maendeleo ya utafiti, ili kuunga mkono juhudi zilizokusudiwa katika kukuza vipaji vya Vijana ndani ya Taifa letu.

*(e)* Kuandaa, kusimamia na kutathmini mipango iliyoanzishwa na Vijana kupitia Jumuiya mbali mbali zilizoanzishwa Zanzibar.

*(f)* Kuhamasisha na kusambaza rasilimali katika kuunga mkono utekelezaji wa mipango ya Vijana na kuimarisha uwezo wa Vikundi na Jumuiya za Vijana.

*(g)* Kuainzisha, kuendeleza na kusimamia miradi yenye faida katika kuunga mkono maendeleo ya Vijana kama itakavyoonekana inafaa.

*(h)* Kupanga na kuendesha Mikutano ya Baraza la Vijana.

## CHANGAMOTO ZA BARAZA LA VIJANA ZANZIBAR

*(a)* Kutokuwa na Ofisi ya kudumu za Baraza la Vijana Zanzibar.

*(b)* Ufinyu wa bajeti katika kutekeleza majukumu ya Baraza la Vijana Zanzibar.

*(c)* Baadhi ya watu kulihusisha Baraza la Vijana Zanzibar na mambo ya kisiasa.

*(d)* Ukosefu wa wataalamu wabobezi wa uanzishaji wa miradi.

*(e)* Ukosefu wa usafiri kwa Mkurugenzi wa Idara ya Vijana.

*(f)* Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri baina ya Baraza la Vijana kutoka katika ngazi ya Wilaya kwenda Taifa.

*(g)* Ukosefu wa soko la ndani na nje kwa bidhaa zinazozalishwa na Jumuiya za Vijana.

*(h)* Ukosefu wa mitaji katika kuendekeza shughuli za Vijana Zanzibar.

*(i)* Kutokuwepo kwa makabidhiano baina ya JKU na Baraza la Vijana kwa Miradi ya ‘Green House’ kwa Unguja na Pemba.

*(j)* Ukosefu wa elimu ya miradi ya uzalishaji kwa vijana wanaojiunga na Vikundu vya Vijana katika Mikao yetu kuipitia Wilaya na Shehia.

*(k)* Kutokufanyika kwa Upembuzi Yakinifu kwa miradi ya maendeleo inayopelekwa kwa Vijana.

## MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

*(a)* Kamati inalipongeza Baraza la Vijana Zanzibar kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii kwa kuanzisha Kongamano Maalum la Utalii kwa Vijana, ili kuweza kuwasaidia vijana wetu kupata elimu inayohusiana na utalii na baadae kuweza kujiari wenyewe bila ya kusubiria kuajiriwa.

*(b)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo kuandaa timu ya wataalamu katika uanzishaji na usimamizi wa miradi ya

maendeleo ya Vijana, kwani Kamati imebaini miradi mingi iliyoanzishwa kupitia Baraza la Vijana haikufanikiwa kutokana na kukosekana kwa utaalamu na usimamizi ulioimara katika Vikundi vinavyopelekewa miradi hiyo.

*(c)* Kamati pia inaishauri Serikali kupitia Baraza la Vijana kuandaa utaratibu wa kukutana na vijana katika Wilaya na Shehia, ili kutoa elimu juu ya umuhimu wa kujiunga na Baraza la Vijana pamoja na kuwaelezea muundo, kazi na majukumu ya Baraza hili.

**MRADI WA "GREEN HOUSE"**

Katika mwezi wa Januari, 2021 Kamati ilifanya ziara katika maeneo matatu ambapo miradi ya "*Green House"* imetekelezwa kupitia Baraza la Vijana, maeneo yenyewe ni Koani Wilaya ya Kati, Donge Muwanda Wilaya ya Kaskazini "B" na Pangeni Wilaya ya Kaskazini "A".

Hata hivyo, kwa masikitiko makubwa Kamati katika kutekeleza kazi zake kwa kipindi cha robo ya pili ilipata bahati ya kutembelea utekelezaji wa mradi huo na kufanya ziara katika baadhi ya "Green House" kwa upande wa Pemba na Unguja, lakini kwa upande wa Unguja hakuna hata "Green House" moja iliyokamilika kwa wakati ambapo hadi ripoti hii inawasilishwa Barazani bado Ujenzi wa Mradi huo haujakamilika na ukizingatia muda wa mkataba umeshapita na fedha zote zimeshalipwa kwa ajili ya utekelezaji wa Mradi huo. Hali inayopelekea fedha nyingi za Serikali kupotea bila ya mafanikio yoyote kwa Vijana na Taifa kwa ujumla.

Aidha, Kamati ilipochunguza kwa undani zaidi waligundua kuwa Mradi huu walikabidhiwa JKU na kwa wakati huo hawakuwa na ujuzi wa kutosha wala utaalamu wowote unaohusiana na uanzishaji wa "Green House".

Sambamba na hilo, Kamati haikufurahishwa na matumizi mabaya ya fedha za Serikali katika mradi wa “Green House” kumi na tisa (19) kwa Unguja na Pemba ambapo fedha yote iliyotengwa kwa utekelezaji wa Mradi huu ilikuwa Shilingi Milioni 528,000,000.

**CHANGAMOTO ZA MRADI WA “GREEN HOUSE”**

*(a)* Kuchelewa kukamilika kwa Mradi wa “*Green House”*.
*(b)* Vijana kutopatiwa taaluma kabla ya kuanza utekelezaji wa mradi huo.
*(c)* Ufuatiliaji wa miradi ya Vijana kwa Viongozi wa Taifa wa Baraza la Vijana pamoja na Uongozi wa Wizara hakuwa vizuri.
*(d)* Kutoshirikishwa Vijana katika Mradi huu tokea katika hatua za awali.
*(e)* Kushindwa kufanya kazi kwa visima vyote vilivyochimbwa katika mradi huu.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inaishauri Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ kuzirudisha fedha zote waliokabidhiwa za uchimbaji wa Visima katika Mradi wa Ujenzi wa "Green House" zote 19 kwa Unguja na Pemba.
*(b)* Vile vile, Kamati inawashauri Viongozi wa Wizara pamoja na Baraza la Vijana kushirikiana kwa pamoja katika kuwapatia taaluma sahihi na kwa wakati muafaka Vijana kuhusiana na miradi ambayo inakusudiwa kutekelezwa katika maeneo yao, kwa lengo la kuweza kuitekeleza kwa ufanisi zaidi na kuweza kuleta tija kwa Vijana wenyewe, Baraza pamoja na Taifa kwa ujumla.

*(c)* Pia, Kamati inaiomba Wizara pamoja na Baraza kuifuatilia kwa karibu miradi ya Baraza la Vijana na kuhakikisha kwamba inafikia malengo ya uanzishwa wake. Sambamba na hilo ikiwa ni miongoni mwa utekelezaji wa Ilani ya CCM katika kuwapatia ajira vijana kupitia masuala tofauti ikiwemo Kilimo, Ufugaji, Uvuvi, Biashara pamoja na Ujasiriamali kwa ujumla.

*(d)* Kamati, inapendekeza maeneo yote yaliojengwa "*Green House"* yawe Shamba Darasa kwa Wilaya na maeneo husika, kwa ajili ya kuweza kupata taaluma vijana wengi zaidi na baadae kuweza kuanzishwa "*Green House* " zao wenyewe kwa kujipatia ajira bila ya kusubiri ajira kutoka Serikalini.

*(e)* Kamati, inapendekeza kufanywa utafiti mwanzo kabla ya kuibua Miradi ya Maendeleo ya Vijana pamoja na kuwashirikisha Vijana kikamilifu katika hatua zote za uanzishaji wa miradi hiyo ndani ya maeneo yao, ili kuondokana na changamoto zilizojitokeza katika utekelezaji wa Mradi wa "Green House".

## D. PROGRAMU YA MAENDELEO YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Programu hii imeundwa na Programu Ndogo mbili ambazo ni Uimarishaji, Uhifadhi, Ubunifu na Uendelezaji wa Utamaduni, Sanaa na Ubunifu pamoja na Ukuzaji na Uendelezaji wa Shughuli za Michezo.

### I. PROGRAMU NDOGO YA UIMARISHAJI, UHIFADHI, UBUNIFU NA UENDELEZAJI WA UTAMADUNI NA SANAA

Katika ufuatiliaji wa utekelezaji wa Programu Ndogo hii Kamati pia ilipata fursa ya kukutana na baadhi ya Taasisi ambazo zipo chini ya usimamizi wa utekelezaji wa Programu hii.

## AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ni kiungo kati ya wamiliki wa hakimiliki na Serikali. Afisi hii ina jukumu la kusimamia Sheria ya Hakimiliki Nam.14 ya Mwaka 2003 kwa pamoja na mambo mengine; kusajili, kukusanya pamoja na kugawa mirabaha kwa wamiliki husika wa hakimiliki waliosajiliwa.

**Muundo wa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki Zanzibar ni kama ifuatavyo:**

Bodi ya Hakimiliki ni Mamlaka ya juu ya Kisheria iliyoundwa chini ya kifungu cha 43(1) cha jaduweli ya Sheria ya Hakimiliki. Bodi hii imepewa uwezo wa kuelekeza, kusimamia utendaji wa Afisi kwa shughuli za kila siku na kufanya maamuzi sahihi yanayohusu maslahi ya Afisi ya Jumuiya ya Hakimiliki (COSOZA).

Afisi ya Msajili wa Hakimiliki ina jumla ya vitengo vitano (5) na Ofisi ya Pemba kama hivi ifuatavyo:-

*(i)* Kitengo cha Usajili na Kumbukumbu;
*(ii)* Kitengo cha Kazi za Maandishi;
*(iii)* Kitengo cha Leseni na Ukaguzi;
*(iv)* Kitengo cha Sheria;
*(v)* Kitengo cha Utawala na Fedha; na
*(vi)* Ofisi ya Pemba.

## CHANGAMOTO ZA AFISI YA MSAJILI WA HAKIMILIKI

*(i)* Uharamia wa kazi za hakimiliki, uharamia wa hakimiliki unatokea pale ambapo kazi za Sanaa zinaghushiwa na kutumika kinyume na Sheria jambo ambalo linawakosesha wasanii haki zao.

*(ii)* Ugumu wa kufanya malipo ya mirabaha kwa watumiaji wa kazi za Hakimiliki kibiashara, wakiwemo wawekezaji wa wazawa, baadhi ya mahoteli, vituo vya Utangazaji vya Umma na Binafsi, Taasisi za Elimu, Vyombo vya Usafiri wa Baharini na Kumbi za Burudani.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inatoa pongezi kwa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki kwa kufanya kazi kwa juhudi na maarifa licha ya kukabiliwa na mazingira magumu ya utendaji wa kazi zao za kila siku. Hivyo, Kamati inawaomba kuendelea kuwa wazalendo na kufanya subira wakati Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na Serikali kuu imo kwenye mipango mizuri zaidi.

*(b)* Aidha, Kamati imefurahishwa na taarifa ya watendaji wa Afisi ya Msajili wa Hakimiliki kuwa wako vizuri kiutendaji hasa katika upatikanaji wa mafunzo ya ndani ya kazi, ambapo kila baada ya muda wanapatiwa mafunzo ya kitaifa, kikanda pamoja na kimataifa kwa sababu Afisi ina mashirikiano ya kitaifa, kikanda pamoja na kimataifa na Taasisi au Mashirika tofauti ya ndani na nje na nchi.

*(c)* Kamati inaishauri Afisi ya Msajili wa Hakimiliki kuendelea kuwa na mashirikiano ya karibu na viongozi tofauti wakiwemo Masheha, Madiwani, Wawakilishi, Wabunge, Wakuu wa Wilaya na Mikoa, ili kazi ya kutoa elimu kwa wasanii pamoja na jamii kwa jumla iweze kufanyika kwa ufanisi zaidi kwa kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, (Redio Jamii), televisheni, magazeti pamoja na mitandao ya kijamii.

*(d)* Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuipatia Afisi ya Msajili wa Hakimiliki rasilimali watu na vifaa kwa ajili ya kuweza kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, kwani hivi sasa kazi zinafanyika lakini sio kwa ufanisi kutokana na hali uhaba au uchache wa rasilimali hizo.

*(e)* Kamati, inatoa rai kwa Taasisi za Elimu ya Juu kama vile *SUZA, SUMEIT, ZU* na nyengine kulipia kazi za maandishi zinazotumika kwenye taasisi hizo, ambapo watunzi au waandishi wa vitabu pamoja na kazi nyengine za maandishi wamejisajili katika Afisi ya Msajili wa Hakimiliki, kwa lengo la kuweza kufaidika watunzi ama waandishi hao wa kazi za maandishi kwa kupata mirabaha. Katika hili Taasisi ya '*Karume Institute Science and Technolog'y* imekuwa ni mfano mzuri wa kuigwa, kwani tayari imeshaanza kulipa.

*(f)* Hata hivyo, Kamati inatoa wito kwa wasanii au watunzi pamoja na jamii kwa jumla kufuata mila, silka, desturi na utamaduni wa Zanzibar na kuachana na kufuata utamaduni wa nje ya Zanzibar, yaani utamaduni wa Kimagharibi ambao hauendani na utamaduni wa Kizanzibari, ambapo utamaduni ni utambulisho wa mtu, kwa sababu utamaduni unajumuisha mambo tofauti yakiwemo lugha, mavazi, vyakula pamoja na mengine.

## BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR (BAKIZA)

Baraza la Kiswahili la Zanzibar (BAKIZA) ni Taasisi ya Serikali iliyoundwa kwa mujibu wa Sheria Namba 4 ya 2004 ya Baraza la Wawakilishi la Zanzibar. Lengo kuu la kuundwa chombo hiki ni kukuza na kushajihisha maendeleo na matumizi ya Lugha ya Kiswahili hapa Zanzibar, Tanzania kwa ujumla na nje ya Tanzania.

**Shughuli za Baraza la Kiswahili**

Baraza la Kiswahili linatekeleza majukumu yake kama ilivyoelekezwa kwenye Sheria. Miongoni mwa majukumu hayo ni haya yafuatayo:-

*(i)* Kushajihisha matumizi ya Lugha ya Kiswahili katika shughuli za Serikali na Sekta nyengine za Umma kwa ujumla;

*(ii)* Kuelimisha jamii juu ya matumizi sahihi, fasaha na sanifu ya Lugha ya Kiswahili kupitia vyombo vya habari ikiwemo redio, televisheni, magazeti, makala katika majarida;

*(iii)* Kuwashajihisha na kuwajengea uwezo watunzi na waandishi chipukizi, ili waandike na kutunga kazi zenye ubora, sambamba na kuwaenzi wasanii wakongwe;

*(iv)* Kutoa huduma ya kutafsiri miswada, makala, sera na nyaraka za Taasisi na watu binafsi kutoka katika Lugha ya Kiswahili kwenda Lugha nyengine na kutoka Lugha nyengine kwenda Lugha ya Kiswahili pamoja na kutoa ithibati kwa kazi zilizotafsiriwa nje ya Baraza;

*(v)* Kutoa huduma za ushauri na uhariri wa miswada ya vitabu vya Kiswahili vya taasisi, watu binafsi na kuthibitisha usahihi wa matumizi ya lugha kabla ya kuchapishwa na kuwa kitabu;

*(vi)* Kushirikiana na taasisi zinazosimamia Lugha ya Kiswahili kuainisha, kusahihisha na kusanifisha istilahi za Kiswahili;

*(vii)* Kuandika na kuchapisha majarida, makamusi, vitabu na miongozo mengine inayohusu Lugha ya Kiswahili na kuisambaza ndani na nje ya nchi;

*(viii)* Kuandaa na kuendesha mafunzo, mijadala, midahalo, makongamano, semina kwa walimu, wanafunzi, waandishi na watunzi wa vitabu, wanahabari na wadau wengine wa Lugha ya Kiswahili;

*(ix)* Kushirikiana na taasisi nyingine zinazokuza Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA KISWAHILI LA ZANZIBAR (BAKIZA)**

*(i)* Uzorotaji wa ukusanyaji wa mapato kutokana na kuwepo kwa kusuasua kwa ununuzi wa vitabu kwa jamii.

*(ii)* Uzorotaji wa uchapishaji wa miswada ya vitabu na makamusi ya lugha moja na mbili ambayo ni muhimu katika kusimamia na kuendeleza lugha ndani na nje ya nchi na utekelezaji wa Sera ya Uchumi wa Buluu.

*(iii)* Kutokuwepo kwa jengo lenye hadhi ya Lugha ya Kiswahili lenye ukumbi, maktaba na maduka ya vitabu kwa ajili ya kuuza vitabu.

*(iv)* Kutoitumia fursa ya Lugha ya Kiswahili nje ya nchi kwa kuuza vitabu kwa kutumia Huduma ya Mtandao (Online na Mobile Market).

*(v)* Kuchelewa kiingizwa kwa fedha za 'OC' kwa wakati hali inayopelekea Baraza kushindwa kutekeleza majukumu waliojipangia.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuliingizia fedha za 'OC' Baraza la Kiswahili kwa wakati na kwa mujibu wa bajeti kwa lengo la kuweza kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

*(b)* Kamati inalishauri Baraza la Kiswahili la Zanzibar kuitumia vizuri fursa ya Lugha ya Kiswahili ndani na nje ya Tanzania kwa kufanya utafiti kuhusu soko ikiwemo Qatar, Misri, Sudan Kusini pamoja na nchi nyengine, ili kuweza kutanua soko lao na kupata mapato mengi zaidi.

*(c)* Vile vile, Kamati inapendekeza kwa Baraza la Kiswahili la Zanzibar kutumia fursa ya Lugha ya Kiswahili nje ya nchi kwa kuuza vitabu kwa kutumia Huduma ya Mtandao (Online na Mobile Market).

*(d)* Kamati inalishauri Baraza la Kiswahili la Zanzibar kuwa wabunifu katika kutafuta wateja kwa ajili ya kununua bidhaa zao tofauti ikiwemo vitabu, makamusi, makala na nyengine kwa kuwafuata wateja sehemu zao za kazi.

Mfano mzuri, Shirika la Mkuki na Nyota lilifika katika Ofisi za Baraza la Wawakilishi mnamo mwezi wa Mei, 2021 kwa ajili ya kuuza vitabu tofauti kama vile vitabu vya Mhe. Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Marehemu Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, Mhe. Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mzee Ali Hassan Mwinyi na Mhe. Rais wa Awamu ya Tatu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Hayati Benjamin William Mkapa.

## BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI (BASSFU)

Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) ni Taasisi ya Serikali ambayo imeundwa kwa mujibu wa Sheria Nambari 7 ya Mwaka 2015 na lipo chini ya Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo. Baraza limefuta Sheria mbili ambazo zilijulikana kama Sheria Nambari 6 ya 1983 ya Baraza la Sanaa na Muziki na Sheria Nambari 1 ya 2009 ya Bodi ya Sensa ya Filamu na Sanaa na Maonesho. Lengo kuu la kuunganishwa Sheria hizi ni kuimarisha utendaji wa shughuli za kijamii katika maendeleo ya Utamaduni na Sanaa Zanzibar.

### Majukumu ya Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU)

Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni miongoni mwa majukumu yake ni haya yafuatayo:-

*(i)* Kuvitambua na kuvisajili vikundi vyote vya Sanaa na Vyama vya Sanaa vilivyopo Zanzibar;

*(ii)* Kuhifadhi, kulinda na kuimarisha mila, silka na maadili ya utamaduni wa Zanzibar;

*(iii)* Kuimarisha Sanaa ya ndani na maonesho ya kitaifa na kimataifa na kusaidia mafunzo na utafiti;

*(iv)* Kusaidia ushiriki wa kikundi au mtu binafsi katika kuwakilisha Zanzibar katika shughuli za Sanaa ndani au nje ya Zanzibar;

*(v)* Kuweka utaratibu mzuri wa kuwatambua, kuwapa tunzo wasanii wa zamani, ambao wamechangia maendeleo ya kazi za Sanaa Zanzibar;

*(vi)* Kuhakikisha kwamba filamu zote zilizorikodiwa nje ya Zanzibar zenye lengo la kuoneshwa hadharani;

*(vii)* Kukagua matangazo ya burudani yanayotolewa kwenye magari na mabango ya biashara; na

*(viii)* Kuthibitisha maombi kwa vikundi vya Wasanii kutoka nje ya Zanzibar vinavyotaka kufanya shughuli zao Zanzibar.

**CHANGAMOTO ZA BARAZA LA SANAA, SENSA YA FILAMU NA UTAMADUNI (BASSFU)**

*(i)* Kasi ya maendeleo ya Sayansi na Teknolojia imeendelea kuathiri maendeleo ya Sanaa ikiwemo mila, silka na desturi na utamaduni wa Zanzibar. Baadhi ya vijana wetu wanatumia vibaya Teknolojia ya mawasiliano na kuathiri kulinda mila na desturi zetu.

*(ii)* Uelewa mdogo wa baadhi ya wasanii na watumiaji wa sanaa katika kulinda haki za wasanii.

*(iii)* Ukosefu wa usafiri wa uhakika katika kutekeleza majukumu ya kila siku hasa Pemba na Ofisi za Wilaya.

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(i)* Kamati inalishauri Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) kuzidisha juhudi katika kutoa elimu kwa jamii kwa kutumiA njia tofauti ikiwemo vyombo vya habari, mikutano katika Shehia pamoja na sehemu nyengine kuhusu namna bora ya kulinda, kuhifadhi na kudumisha mila, silka, desturi pamoja na utamaduni wa Zanzibar.

*(ii)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango kuliingizia fedha za OC Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) kwa wakati na kwa mujibu wa bajeti, ili liweze kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

*(iii)* Aidha, Kamati inalishauri Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU) kuongeza bidii na maarifa katika kutoa elimu kwa wasanii, wabunifu kuhakikisha kwamba wanaelewa haki zao pamoja na wananchi kutumika kazi za sanaa kwa mujibu wa utaratibu uliopo kwa ajili ya kuwawezesha wasanii pamoja na wabunifu kunufaika na kazi zao.

*(iv)* Kamati inapendekeza kwa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filamu na Utamaduni (BASSFU), kuwapa taaluma watendaji tofauti kuhusu utaratibu wa utoaji wa

vibali pamoja na udhibiti wa ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuongeza mapato kwa Baraza la Taifa kwa ujumla.

## C. PROGRAMU KUU YA UTAWALA, UENDESHAJI NA MIPANGO KATIKA SEKTA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO

Programu hii ina jukumu la kusimamia na kuratibu Mipango Mikuu, Sera na Tafiti pamoja na kuratibu na kusimamia Shughuli za Utawala na Uendeshaji mzuri wa Rasilimali watu katika Wizara.

**CHANGAMOTO KATIKA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU**

*(a)* Kutokuwepo kwa usimamizi madhuti katika utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo inayohusu Vijana hii imebainika na Kamati wakati wa ziara za kufuatilia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali. Mfano wa Miradi hiyo, Mradi wa Ujenzi wa "Green House" 19 kwa Unguja na Pemba, Mradi wa Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vilivyojengwa katika Wilaya 5 kwa Unguja na Pemba ambapo Unguja 3 na Pemba 2 na Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Studio ya ZBC Pemba.

*(b)* Kutokuwepo kwa mashirikiano mazuri ya kiutendeaji baina ya Viongozi wa Juu wa Wizara na Watendaji wa chini. suala hili lilionekana na Kamati wakati wa taarifa za utekelezaji wa Bajeti kwa upande wa Pemba.

*(c)* Uwepo wa uelewa mdogo wa matumizi ya Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma kwa baadhi ya Wakuu wa Idara kwa upande wa Pemba.

*(d)* Uhaba wa rasilimali watu hususan wataalam wabobezi katika fani tofauti wanaohitajika katika uendeshaji wa shughuli za kila siku za Wizara hii.

*(e)* Kutokuwepo kwa Muundo wa Utumishi katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC).

*(f)* Baadhi ya Taasisi za Serikali kutotekeleza agizo la Serikali la kupeleka kazi zao za Ofisi kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali (ZAGPA).

*(g)* Kuwepo kwa bei ndogo ya Gazeti la Zanzibar Leo kwa muda mrefu.

*(h)* Kutokuwepo kwa stahiki kwa baadhi ya Wakuu wa Vitengo na watendaji wa chini ambazo wanastahiki kupatiwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Ikiwemo "Over times" Posho la Mazingira Magumu pamoja na Posho la Kushika Nafasi za Uongozi,

**MAONI/USHAURI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI**

*(a)* Kamati, inaishauri Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kufanya utafiti mwanzo kabla ya kuibua miradi ya vijana pamoja na kuwashirikisha vijana wenyewe wa maeneo husika, kwa lengo la kuwa na miradi mizuri na itakayoweza kuleta tija kwa Vijana na Taifa kwa ujumla pamoja na kuweza kunusuru upotevu wa fedha nyingi za Serikali.

*(b)* Aidha, Kamati inaushauri Uongozi wa Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kutatua tatizo la rasilimali watu pamoja vifaa kwa Shirika la Utangazaji Zanzibar (*ZBC*), ili kuwaweza kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na weledi.

*(c)* Kamati, inaishauri Serikali kuhakikisha kwamba Taasisi zote za Serikali zinapeleka kazi zake kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar (ZAGPA) pamoja na kulipa kwa wakati kwa ajili ya Wakala kuweza kujiendesha na kujitegemea wenyewe na kufikia malengo iliyojipangia.

*(d)* Pia, Kamati inaiomba Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuzidisha mashirikiano na Taasisi ya *Tanzania Horticultural Association*

*(TAHA)*, kwa ajili ya kupatiwa elimu pamoja na utaalamu kuhusu masuala ya kilimo na mbegu bora kwa Mabaraza ya Vijana kwa lengo la kulima kwa kutumia utaalamu na maarifa mapya, ili kuweza kupata mafanikio makubwa zaidi ya kulima eneo dogo, muda mdogo lakini mafanikio yenye tija kubwa.

*(e)* Vile vile, Kamati inaishauri Serikali kupitia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kuandaa mpango madhubiti wa usimamizi na ufuatiliaji wa Ujenzi wa Miradi ya Maendeleo inayohusu Wizara, ili kuondoa changamoto ya uchelewaji wa ukamilishaji wa miradi hiyo.

*(f)* Pia, Kamati inaiomba Serikali kuliangalia upya suala la upandishaji wa bei wa Gazeti la Zanzibar Leo, ambapo bei iliopo ni ndogo na ya muda mrefu na imeshapitwa na wakati ukilinganisha na magazeti mengine nchini Tanzania.

*(g)* Kamati inaiomba Serikali kupitia Tume ya Utumishi Serikalini kukaa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo kulishughulikia kwa haraka iwezekanavyo suala la kutokuwepo kwa Muundo wa Utumishi katika Shirika la Utangazaji Zanzibar (ZBC), hali inayowapelekea watendaji kukosa baadhi ya stahiki zao zilizopo kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma.

*(h)* Kamati inaishauri Wizara ya Habari,Vijana,Utamaduni na Michezo kwa kushirikiana na Idara ya Utumishi ya Wizara kuandaa mpango wa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watendaji wote wa Wizara hii, ili kuendana na mabadiliko yanayojitokeza kwa Tasnia ya Habari, Utamaduni na Michezo.

# SEHEMU YA TATU

## HITIMISHO

Kamati ya Ustawi wa Jamii ya Baraza la Wawakilishi inawapongeza kwa dhati Mawaziri, Makatibu Wakuu, Manaibu Makatibu Wakuu pamoja na watendaji wote kwa ujumla wa Wizara zote tatu zinazosimamiwa na Kamati hii kwa mashirikiano makubwa waliyoipatia Kamati kwa kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake ya Kikatiba na Kikanuni.

Aidha, Kamati inatoa shukurani za kipekee kwa Maafisa Wadhamini wa Wizara hizi pamoja na wasaidizi wao wote kwa mashirikiano mazuri waliyoipatia Kamati wakati wote Kamati ilipokuwa Kisiwani Pemba katika kutekeleza majukumu yake.

Vile vile, Kamati pia inatoa Pongezi za Dhati na Maalum kwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ Tanzania Bara kwa mashirikiano yao ya dhati kwa kuwa bega kwa bega na Kamati wakati ilipokuwa Katika ziara za kiutendaji na kimafunzo huko Dar-es-Salaam.

Mwisho, na kwa umuhimu mkubwa Kamati inampongeza kwa dhati Spika wa Baraza la Wawakilishi Mhe. Zubeir Ali Maulid, Naibu Spika Mhe. Mgeni Hassan Juma, Katibu wa Baraza la Wawakilishi Ndg. Raya Issa Msellem, Mratibu wa Kamati Ndg. Khamis Hamadi Haji pamoja na wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa kuiwezesha vyema Kamati kutekeleza majukumu yake na kuweza kutayarisha ripoti yake kwa mwaka 2021/2022. Kamati inashauri mashirikiano hayo yaendelezwe kwa kipindi chote kinachofuata.